# Kutambua Siku Yako Na Ujumbe Wake

Jeffersonville, Indiana, Amerika

Julai 26, 1964A

1 Habari za asubuhi marafiki. Hebu tubakie tukiwa tumesimama kwa kitambo kidogo.

Mungu mpenzi, sisi katika huu msukumo na harakati za maisha, tumetulia hapa kwa hiki kitambo kidogo kijacho au saa, chochote kile kiwacho, kile ambacho umetupa, ili kukusifu na kukutukuza Wewe, kuhubiri Neno Lako, kukujua Wewe vizuri zaidi, hiyo … Ndiyo sababu tumekusanyika asubuhi hii. Tunakushukuru Mungu kwa kuwa kuna watu walio tayarina wamejiandaa kuja kusikiliza. Bila kujali hali na wakati tunaoishi, bado wanaamini. Na tunakushukuru kwa ajili yao.Mungu tunakushukuru kwa ajili ya nguvu Zako kuu za uponyaji, ahadi za Neno Lako. Jinsi mioyo yetu inavyowaka tunaposikia hizi shuhuda! Namna zote za mateso zilizoletwa juu ya wana wa binadamu! Wewe, na neema Yako na nguvu, na kwa ahadi Yako, umewaponya.Nao wako hapa, wakishuhudia, wakimsifu Mungu. Tunakushukuru kwa hili. Na sasa,leo tusikie Ujumbe ule Wewe uliotupa kwa ajili ya saa hii. Tunaposoma katika Neno Lako, hebu utupe maana ya kile tunachokisoma. Hebu mapenzi Yako yatimizwekatika mambo yote, kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. Mnaweza kuketi.

2 Ni heshima kuwa hapa asubuhi hii. Nina furaha mno kwenu ninyi nyote. Na Ndugu Woods, Ndugu Roy Roberson, ndugu wengi wengine, wamefanya kazi kwa uaminifu siku mbili zilizopita, kuliwekea vifaa vya kurekebisha hali ya joto hili jengo kwa ajili ya hili kusudi, kwa sababu Jumapili iliyopita waliona jinsi mlivyotaabika. Nao walikuwa na fedha kidogo katika hazina ya kanisa, na wakaenda kufanya kazi na kuziweka kazini kuwafanya mjisikie vizuri, kwa zile fedha mlizoweka katika matoleo, mnaweza kuketi, na kusikiliza Ujumbe. Leo kuna baridi zaidi kuliko ilivyokuwa kule. Kwa hiyo tunamshukuru Mungu na ninyi watu, kwa ajili ya nafasi hii.

Nafurahi … Ndugu Roy Bordres … Alitaka kukaa kule nyuma asubuhi hii. Na nilimwambia achukue kiti chake na kuketi hapa pamoja na hawa wahudumu, lakini hakuweza kufanya hivyo. Na nyote mnavyojua, Ndugu Borders anatuwakilisha katika shamba la huduma. Ni furaha kuwa na Ndugu Borders ndani, na wahudumu wengine wengi na marafiki.

3 Katika juma lote hili nili-nilifikiri, na kusema, "Nitakapofika pale Jumapili, nitamtambua kila mhudumu, kila mtu." Ndipo unapofika pale, umechukuliwa mno katika Ujumbe, hadi unasahau karibu kila kitu, kilikuwa nini.

Sasa inanipasa kurudi Arizona. Inanipasa kurudi Jumatatu ijayo, juma moja; kurudi Tucson, kuwapeleka watoto shuleni. Na nitarudi baada ya hilo. Na mke wangu inampasa kuwa kule mapema, ili aanze … kuorodhesha watoto, majuma mawili kabla shule haijaanza. Na nita … ndipo nitarudi hapa nikae kitambo.

Na sasa huu ni wakati wangu wa likizo. Kama mnavyojua, nimehubiri tangu Desemba; Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni na Julai. Sasa, Mungu akipenda, na sio wito wowote maalum, haya ni majira ambayo na-na-napumzika, likizo yangu. Nakwenda kuwinda, Na nina …

4 Sasa ikiwa Bwana angeniita kwa jambo lingine, hayo mambo hayako nje ya mtazamo. Mungu ni wa kwanza siku zote. Na mimi nataka Yeye awe mtangulizi. Na wewe unamtaka Yeye awe mtangulizi. Lakini basi ikiwa hakuna wito fulani, na hilo likiwa mapenzi Yake, hilo ndilo nitakalofanya sasa kwa miezi kadha ijayo, ni kwenda kuwinda sasa, kujipumzisha. Nina …

Hutambui, kamwe ulimwengu hautajua, kile ningepitia. Unaona? Ni uchovu tu. Haiyumkini Bwana aliwaambia wanafunzi Wake, alipokua akitembea nao, "Nendeni jangwani, pumzikeni kidogo." Unaona? Natambua hilo zaidi, kila siku, na hasa kadiri siku zangu zinavyozidi juu ya nchi, unaona. Ninapozeeka, unalitambua hilo. Ninamsikia mchungaji wetu akisema "amina" kwa hilo pia. Yeye, sisi tunaweza kutambua kuwa sisi sio wavulana baada ya kuvuka umri wa miaka hamsini. Sasa inatupasa kuwa na muda kidogo.

Tunashukuru mno kwa shuhuda tulizozisikia muda mfupi uliopita. Mke wangu alikuwa kule kwa Dada Woods, jana, watu fulani walipokuja kutoka Alabama, mahali fulani kule, na walikuwa wakieleza kuhusu mambo makuu Bwana aliyoyafanya katika ule mkutano, ya watoto wadogo wakiponywa, na mambo mbalimbali, na mambo mengi mno, ambayo … jamani itachukua tu muda mrefu ku-kuweza kuelezea.

5 Basi yanipasa kukumbuka kuwa … Naamini baadhi yao waliniambia kuwa Dada larson amekuwa hapa Jumapili mbili akiwa na mtoto mchanga. Singejua, lakini naamini walisema alikuwa mjukuu wake, labda kwa ajili ya kuwekwa wakfu, akimleta kutoka Chicago. Yule mama amekuwa mwema sana kwetu, na tunamshukuru. Na alimleta mtoto mdogo kutoka Chicago, kwa ajili ya kuwekwa wakfu, ambapo nadhani, anatumia muda mrefu kumtoa kwa ajili ya kuwekwa wakfu, lakini anapenda huyu mtoto awekwe wakfu kwa Bwana. Kwa hiyo ikiwa Dada larson, ninapoongea, ikiwa tu atamleta yule mtoto huku kwa ajili ya hii huduma ya kuwekwa wakfu ...

6 Na ndipo, labda, anapojiandaa, na-nataka kusema kuwa huu umekuwa Ujumbe mgumu zaidi kuliko zote nilizowahi kujaribu kuandaa, hadi usiku uliopita. Juma zima, nilikuwa ninaingia chumbani, kujaribu

kutulia baada ya kupiga na kupokea simu baada ya simu zangu na mengineyo, ku-kujaribu kupata jambo fulani akilini mwangu kwa ajili ya wakati huu. Na wakati ambapo ningekwenda na kupokea simu, si-singeweza hata … Akili yangu ilikuwa tupu. Na, jana nilikwenda kule chumba cha chini. Nilifikiri ilikuwa joto mno, kwa hiyo nilikwenda kule chumba cha chini, nikaketi pale. Na nikajaribu kushika Biblia yangu na kuisoma, na nikaishia usingizini. Ndipo ningeamka na kunywa maji na kujaribu kujitikisa, na kutoka nje na kutembea huku na huku, na kuketi kwenye ngazi.

Mtu fulani anakuja na kunikuta nimevua shati, nimeketi kwenye ngazi; ilikuwa joto mno. Walinipungia mkono. Sikujua kama walinipungia mkono … Mtu fulani, inaweza kuwa mtu fulani mwenyeji wa mji, au ingeweza kuwa mtu fulani katika kanisa, alinipungia mkono. Na ni-nilikuwa ninawaza sana. Nika-nikatokewa tu na tazamo la haraka gari lililopita pale. Nikapungia mkono.

7 Usiku uliopita niliingia kwenye gari na nikaenda kuelekea Charlestown, nikijaribu kupata kitu fulani. Ilionekana kwamba, Bwana, alitaka kuniambia jambo fulani, lakini nili- … Shetani alikuwa anajaribu kusimama njiani, akinizuia kukifanya. Kwa hiyo nikawaza, "Vema, ikiwa anafanya hilo, nitaendelea kungojea kwa saburi tu, nitaendelea kusubiri tu, nikigonga mlangoni hadi Yeye afungue." Kwa hiyo basi muda kidogo uliopita, au kidogo baada ya saa moja asubuhi hii. Nilikuwa nimeamka mapema kweli.

Jana, nikiwa mgonjwa kidogo, nikijaribu … Nilikuwa nimekula mahindi ambayo hayakuwa yamepatana na mimi vizuri, yalikuwa na pilipili nyingi, na ni-nilikuwa najaribu kuondokana na hilo. Na-na ndipo asubuhi hii, mnamo saa mbili, ilinilitokea kupata Andiko lililonistaajabisha. Na nililitazama Lile Andiko tena na tena. Lilinistaajabisha. Na nikaenda katika Maandiko kulifuatilia, na nilimaliza tu dakika chache zilizopita. Kwa hiyo huenda Bwana ana Ujumbe kwa ajili yetu, asubuhi hii, ambao Shetani amejaribu kuuzuia.

Ungemleta huyo mtoto hapa Dada Larson? [Ndugu Branham anamweka mtoto wakfu. Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] Mungu awe nao na awasaidie.

8 Sasa nimekuwa nikiwachelewesha, Jumapili iliyopita, siku mbili, na nadhani … au, ibada mbili, asubuhi na jioni, na hilo linakuwa gumu kwenu. Nafahamu kuwa … Baadhi yenu inawapasa msafiri mbali sana, na kukosa kufanya kazi kwa siku moja, na kadhalika. Kwa hiyo hata kama tutaondoka Jumapili-Jumapili kwa juma moja, nitatangaza tu ibada ya Jumapili ijayo, Bwana akipenda, unaona, labda kusanyiko lipende iwe kukaa hadi usiku. Unaona? Hilo, hilo ni juu … Mko wengi mno!

Wangapi mngependa bora iwe usiku huu, hebu tuone-tuwe na hizo ibada usiku huu? Sasa, ni bora tukawa nayo Jumapili ijayo, inueni mikono yenu. Jamani, hiyo ni karibu sawa. Uh! [Mtu fulani anasema, "sare, ndugu!-"Mh.] Umesemaje? [Ndugu Ben Bryant anasema, "Na, usiku tuwe nazo mbili."] Sasa, sasa, Ben? [Ndugu Branham anacheka.]

9 Ninao huu Ujumbe, ni mrefu, asubuhi hii, lakini si-sijui tu jinsi … Na najua kuwa huwa nasaidia kuweka sheria za kanisa, lakini pale, ikiwa mtaona, nilisema, "Isipokuwa niwe narekodi." Unaona? Kwa hiyo, hii ni kurekodi. Uh-huh. Kwa hiyo labda tutajaribu kurudi mara mbili, usiku huu na Jumapili ijayo, ndipo tutafanya kama Bwana anapenda, unaona.

Sasa, ikiwa hamkupata ujumbe juma hili, basi mje Jumapili ijayo.Nachukia ninyi kuja mara mbili namna hiyo, lakini najisikia kuwa tunao muda mchache tu zaidi. Na kumbukeni tu, ikiwa wakati utaendelea kuweko, hatutakuwa na fadhila hii kwa muda mrefu sana. Unaona? Kumbukeni, jambo fulani litatokea. Ama sheria itatusimamisha, ama Shetani atatembea miongoni mwenu na kuwatawanya. Siku zote imekuwa hivyo. Unaona? Jambo fulani litatokea, kwa hiyo hebu tushukuru kwa kila dakika tunayokuwa pamoja.

10 Kwa hiyo sasa kwa wale ambao inawapasa kurudi manyumbani kwenu, usiku huu, itakuwa kama Jumapili ilyopita usiku, nilikuwa tu na Ujumbe mdogo mfupi. Na hivyo, ninyi, ikiwa mnautaka kwenye kanda, basi, hakika tutawapelekea kanda ikiwa itawapasa kurudi nyumbani. Au, sio, nitahubiri usiku huu, Bwana akipenda.

Nilikuwa na muhtasari jana, au-au juzi, Ujumbe mdogo nilioandika kutoka kwenye kumbukumbu ya kitu fulani, na ni kutoka muda mrefu. Kuna Jumbe mbili, hata hivyo. Mmoja ni kati ya "Birika Livujayo," au mmojawapo, "Kupanda kwenye upepo na kuvuna kimbunga," Ujumbe wa Injili tu. Asubuhi hii ni kufundisha. Na hivyo, usiku, wa leo, ama nitahubiri juu ya, "Kupanda kwenye upepo na kuvuna kimbunga," ama mmojawapo, " Birika Linalovuja."

11 Na, asubuhi hii nataka kusoma kutoka kwenye Maandiko Matakatifu sasa. Na je mna raha? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Vizuri. Sasa nawatakeni, katika Biblia zenu, mfungue pamoja nami kwenye Kitabu cha Hosea,mnaotamani kusoma. Na hebu tusome aya chache kwenye sura ya 6 ya Kitabu chaHesea nabii. Na tusimame.

12 Mungu mpenzi, hatustahili kuchukua hiki Kitabu mikononi mwetu, kwani tunasoma katika Maandiko kuwa hakuna mtu Mbinguni wala duniani, au chini ya ardhi, aliyestahili au hata kuweza kuchukua kile Kitabu, au hata kukitazama. Lo, pale akaja Mmoja aliye kama mwanakondoo aliyechinjwa; Yeye

alikichukuwa kile Kitabu, kwani Yeye alistahili, na Yeye alivunja Yake Mihuri ile. Na tunamtazamia Yeye asubuhi hii kufunua maana hizi zilizoandikwa katika Kitabu, kwa sababu ni Kitabu cha ukombozi. Wote waliokombolewa wameandikwa ndani mle. Basi na tupate nafasi zetu, asubuhi hii, katika wakati tunaoishi. Kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

> *Njoni, tumrudie Bwana; maana yeye amerarua, na yeye atatuponya; yeye amepiga, na yeye atatufunga jeraha zetu.*
>
> *Baada ya siku mbili atatufufua; siku ya tatuatatuinua, nasi tutaishi mbele zake.*
>
> *Nasi na tujue, naam, tukaendelee kumjua Bwana; kutokea kwake ni yakini kama asubuhi; naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya vuli iinyweshavyo nchi.*
>
> *Ee Efraimu, nikutendee nini? Ee Yuda, nikutendee nini? Kwa maana fadhili zenu ni kama wingu la subuhi na kama umande utowekao mapema.*
>
> *Kwa sababu hiyo nimewakata-kata kwa vinywa vya manabii; nimewaua kwa maneno ya kinywa changu; na hukumu yangu itatokea kama mwanga.*
>
> *Maana nataka fadhili wala si sadaka; na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa.*
>
> *Lakini wao wamelivunja hilo agano kama mwanadamu; huko wamenitenda mambo ya hiana.*
>
> *Gileadi ni mji wa hao watendao maovu, umetiwa rangi ya damu.*
>
> *Na kama vile makundi ya wanyang'anyi wamwoteavyo mtu, ndivyo kundi la makuhani wauavyo katika njia ielekeayo Shekemu; naam wametenda mambo maovu sana.*
>
> *Katika nyumba ya Israeli nimeona jambo bovu kabisa; huko uzinzi umeonekana katika Efraimu; Israeli ametiwa unajisi.*
>
> *Tena, Ee Yuda, wewe umeandikiwa mavuno, hapo nitakapowarudisha wafungwa wa watu wangu.*

Bwana Yesu, toa kutoka Hili, kwa Roho Wako Mtakatifu maana iliyokusudiwa, tunapoendelea kukusubiri zaidi. Katika Jina la Yesu. Amina.

13 Sasa, somo langu asubuhi hii ni Kutambua Siku Yako Na Ujumbe Wake. Tunaona kutoka somo la Jumapili iliyopita, tulipofundisha, Sikukuu ya Baragumu. Na nataka kuomba usikivu wenu, sasa, wakati-wakati wa Israeli ndio saa ya Mungu.

Tunashughulika leo juu ya somo la Jumapili, ambalo nataka mfahamu na mtambue wakati tunaoishi. Tunakaribia tu kumaliza, mnavyoona. Na ndipo, kwa hili, unapaswa kujua saa na wakati hasa, na ishara na Ujumbe utakaoupokea.

14 Sasa, kama tulivyoanza Jumapili iliyopita … Tumekuwa tukinena juu ya kwenda kuhubiri juu ya Baragumu, Baragumu Saba za mwisho za Biblia. Na mimi, ndani yangu mwenyewe, nilidhani zingevunjika kama tu Mihuri. Lakini nimeona kwenye kila ufunguzi wa kila mmoja kumekuwa na tukio kubwa mno. Na kama tulivyohubiri zile Nyakati Saba za Kanisa, na zilikuwa kamilifu mno hadi Roho Mtakatifu Mwenyewe akashuka miongoni mwetu na kulithibitisha, na kuliweka kwenye karatasi, na kulirusha kote katika taifa, na kulionyesha kwenye mwezi mbinguni, na kulithibitisha kwetu, majuma na miezi kabla halijatukia, jinsi ambavyo lingekuwa, kwa ukamilifu. Yeye alifanya lijulikane hapa Hekaluni. Hapa kwenye … katika wakati. Yeye alifanya lijulikane. Kwenye mwezi na jua, Yeye alifanya lijulikane. Na kwa sehemu ya mataifa, kwa wakati huu, Yeye alifanya lijulikane; utawala wa Rumi ulipokuwa unaondoka na kurudi Palestina, yamkini amekuwa papa wa kwanza kurudi tangu (wanadai) Petro awe papa. Sasa, lilikuwa jambo kuu mno.

15 Ndipo tunaona, kabla ya Mihuri Saba kile kilichoficha mafumbo yote. Mimi bila kujua kile nilichokuwa nikichora ubaoni, kwa ajili ya Nyakati za Kanisa. Kamwe sikujua. Mungu anajua. Nililipata tu kwa maono. Nikachora. [Angalia picha namba 4-Mh.] Bila kujua kuwa Mungu mwaka mmoja na miezi sita baadaye, alikuwa anakwenda kulithibitisha angani, kwa kutumia mwezi, na kulipenyeza kwenye magazeti ya taifa. Sikujua hilo. Sikujua kungekuwa na kufunikwa kwa mwezi kimafumbo, kuwakilisha hiki Kipindi cha Laodikia.

Sasa, kwenye magazeti unapata tu nyakati sita. Ni kwa sababu kanisa la Laodikia lilifunikwa kabisa. Na kama ungeona kiroho, kama Mungu alivyoliweka mbinguni. [Angalia picha namba 1-Mh.] Nilivyopangilia katika mchoro hapa duniani, niliacha kanafasi kadogo, kama unavyoona. Hiyo ilikuwa kabla tu ya Wateule halisi hawajaitwa kutoka duniani, ndiyo sababu nilipaweka pale kwa ajili ya kipindi cha saba. Lakini Mungu alipoliweka mbinguni lilikuwa limefunikwa kabisa, ikimaanisha yule wa mwisho ameitwa kutoka Kipindi kile cha Laodikia. Hatujui. Kungekuwa na mahubiri juu yake.

16 Sasa, tazameni tena, kabla ile-ile Mihuri Saba, ambayo sikuwa na wazo kuwa ilikuwa vile. Hapa

Hekaluni. Yeye alinena juu yake, na kunituma Tucson, Arizona, akiwaambia yote ambayo yangetukia. Na kuna mtu aliyeketi hapa, leo, aliyekuwa pale akiona likitukia kikamilifu tu jinsi lilivyosemwa hapa kuwa lingetukia, "Malaika Saba wangekuja." Ndipo magazeti yakaandika hilo, magazeti, nchini kote, "Duara ya Nuru ya Ajabu yenye umbo la piramidi," kama tu nilivyolichora hapa na kuwaonyesha. Liliinuliwa juu kutoka pale wale Malaika walipokuwa wamesimama, na kwenda maili thelathini juu, na lilikuwa maili ishirini na saba kwa mapana; au ama maili ishirini na saba kwenda juu, na maili thelathini kwa mapana, nasahau ilikuwa vipi. Na lilionekana kote nchini, juu tu ya Tucson, Arizona, pale pale lilipotokea, muda ule ule. [Angalia picha namba 5-Mh.]

17 Unaona, Biblia, Mungu sio tu … Hii sio mtu fulani akijaribu ku-kushinikiza kitu fulani kwenu, ili kufunua kwenu mambo ya kiroho yanayohusu saa hii.

Na ndipo Ujumbe uliofuata ulifungua, ile Mihuri Saba, ambayo inafunua mafumbo yote ya Biblia yaliyofichwa, yale Mafundisho na kadhalika. Ambayo, ulimwengu unayashambulia kwa fujo mno siku hizi, wanashambulia Hilo na kusema ni makosa, hili, lile.

Hapa Arizona siku ile, walijaribu kuunganisha kanda, ili kujaribu kunifanya niseme mambo ambayo sikusema. Kumbukeni tu lile ono kuhusu suala la Arizona! Biblia ilisema, "Ilikuwa vyema zaidi kwako wewe uliyekuwa na jiwe shingoni mwako." Na jambo lingine, kwamba, "Yeyote," awe muhubiri au chochote awacho, "atatoa Neno moja kutoka Hilo, au aongeze neno moja kwa Hilo!" Watu wakiweka fasiri yao wenyewe juu ya Neno kama ilivyotolewa, wakijaribu kulifanya liseme jambo ambalo sikusema, na, sio Neno langu; Ni Neno lake. "Nani ataongeza kwalo, au kuondoa!"

Na kisha, katika lile ono, tuliona hawa manabii wakivurumisha kuja chini kwa kasi, kama nilivyowaeleza, naamini, Jumapili kadha zilizopita. Yote yatakuwa. Nilisema, "Kaeni tu mbali na hilo." Maadam napigana nalo, basi Mungu hawezi kupigana nalo. Lakini hebu tumwachie Yeye awe nalo. Yeye Ndiye Ambaye analishughulikia. Unaona?

18 Sasa tuliona, Jumapili ilyopita, kulikuwa na … nikihubiri juu ya siku za sikukuuu. Na kulikuwa na sikukuu ya Pentekoste. Na kati ya sikukuu ya Pentekoste na sikukuu ya baragumu, hicho kilikuwa kipindi kirefu; siku hamsini kamili kati ya pentekoste na sikukuuu ya baragumu. Na siku hamsini, ambapo pentekoste maana yake "hamsini." Ilikuwa ni kutikisa mganda, au ile … Mavuno ya kwanza yaliletwa ndani. Na tunaona ilikuwa katika mfano kule nyuma, kwa mavuno ya kwanza ya asili, yakiwakilisha mazao ya kwanza ya Roho Mtakatifu yatakayomwagwa juu ya watu. Na tunakuta, basi, kuwa zile siku hamsini zilipokelewa na Mataifa ambao, "Mungu aliita watu kutoka Mataifa kwa ajili ya Jina Lake," sikukuu ya pentekoste. Na tumekuwa tukipitia ile sikukuu ndefu ya Pentekoste.

Sasa, kwa kweli, kutoka kwenye siku hamsini, kungekuwa Sabato saba kamili. Na Sabato saba ziliwakilisha Vipindi Saba vya Kanisa, kuitwa katika wakati wa sikukuu ya pentekoste, ya Pentekoste, kuita watu kutoka Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Sasa, mwishoni mwa hizi Sabato saba, ambazo zimekuweko, kungekuwepo Siku ya Upatanisho, ambayo ilikuwa Baragumu Saba. Na zile Baragumu Saba ilikuwa ni kuitisha watu kwenye siku ya maombolezo, kurudi kwenye Dhabihu, au, Upatanisho. Na tunakuta basi, kuwa, Israeli, Baragumu saba zilihusika tu na Israeli.

19 Na, ndipo, sababu Yeye hangeniruhusu nihubiri zile Baragumu Saba. Hata nilikuwa tayari kulitangaza, nilikuwa tayari na ukumbi na kila kitu kuingia, ili kuhubiri Baragumu Saba. Na nikasema, "Kuna jambo linalonitatiza vibaya sana," nilisema. Tuliendelea kufanya kazi, na Billy na sisi sote, tukijaribu kuweka kila kitu tayari kwa ajili ya jengo lenye vifaa vya kurekebisha hali ya hewa, kwa ajili ya hili juma linalofuata, kwa ajili ya Baragumu Saba; tukiwa na siku kumi au siku nane, tulikuwa na ukumbi wa shule. Lakini Roho Mtakatifu hakuniruhusu kufanya hilo, kwa ajili ya sababu fulani, na nilishangaa ni kwa nini. Na nilipoingia ndani kuomba, nilimwambia mke wangu, "Naingia ndani." Na kwa unofu wa moyo nilipiga magoti mbele za Mungu, kuomba. Na Yeye alinifunulia kwamba zile Baragumu Saba zilitoa sauti zao chini ya Muhuri wa Sita, na nimekwishazihubiri, kiungu. Unaona, ni mkono wa Mungu, jambo lote. Linawahusu Israeli, na tulilichukuwa chini ya Muhuri wa Sita; ninyi nyote mlio nalo, juu ya mateso ya Wayahudi.

20 Wakati wa Mataifa umekuwa katika hii sikukuu ya pentekoste. Zile Baragumu chini … zote zilitoa sauti zake chini ya Muhuri wa Sita. Na tuliongelea Jumapili iliyopita, chini ya sikukuu ya baragumu, ikiwa nyote mnataka kulielewa. Ilikuwa ifanye nini? Kuwaharakisha Wayahudi, toka pande zote za ulimwengu kurudi kwenye nchi yao. Lazima liwepo. Na kufunguliwa kwa Mihuri, chini ya Muhuri wa Sita, na chini … Zile Baragumu Saba zilitoa sauti katika ule-ule Muhuri wa Sita.

Sasa, Ujumbe wa malaika wa saba ni kufumbua fumbo la ile Mihuri, akiita watenda kazi wa Mataifa wa saa kumi na moja ili wapate ujira ule ule walioupata wale watenda kazi wa saa moja. Unaona? Sasa, Yesu alilifundisha. Alisema kulikuwa na watu waliokwenda kwenye mavuno. Walikuwa wameajiriwa. Na walipovuna, wale wa mapema asubuhi walipokea wa-wa-wakati, fedha ya malipo ya siku. Na baadaye mchana, mwingine alikuja na kwenda kufanya kazi. Na, ndipo kwenye saa kumi na moja, hiyo ni saa ya mwisho kwa mchana, mwingine akaja na kupokea ujira ule ule waliopokea wa saa moja ya siku ile, saa ya mwisho.

Ni kamilifu mno, jinsi wale wajumbe wa saa ya kwanza wakiwa na Neno, wakiwa na Injili, wakiwa na ile Kweli, walikuja katika ile siku ya Pentekoste. Ndipo kukawa na kipindi cha giza kilichowafunika. Ndipo katikati ya siku, Luther, na Wesley, na wengineo, wakaja. Na ndipo kutakuwa na Ujumbe wa wakati wa jioni, na kupokea kile kile walichopokea hapo mwanzo. Ujumbe wa wakati wa jioni ni kurejesha tena, kurejesha kitu kile kile tena.

21 Na kumbukeni lile ono juma lililopita, lile wakati Bibi Arusi alikuwa … mwonekano wake wa awali. Kulitokea Bibi arusi mdogo, anayependeza sana, katika ono. Na mimi, bila kuliwazia; nikiwa nimekaa pale, nikitazama nje. Na pale akaja Bibi arusi. Nilisikia Sauti pembeni mwangu, ikasema, "Huu ni mwonekano wa Bibi arusi." Naye akaja. Nilimwona, jinsi alivyokuwa, anapendeza mno, mwenye sura nzuri, kijana. Alikuwa anatembea kwa hatua kama alivyoweza, sio kama mwendo wa gwaride; kwa hatua za-za mwanamke tu, jinsi walivyotembea kwa madaha, kama mwanamke. Hivyo ndivyo alivyokuwa anatembea, akija upande wangu wa kushoto kwa upande huu, naye akaondoka machoni pangu.

22 Ndipo Yeye akanigeuzia upande wa kulia, na akanionyesha kila kanisa kama walivyotokea kwenye vipindi. Na, lo, uchafu ulioje! Nayule wa mwisho alikuwa wa kipindi hiki, kanisa la siku ya mwisho, ambalo liliongozwa na mchawi. Na walikuwa wamevaa kiovu, walionekana wachafu! Na walikuwa wanatembea kwa mapigo ya kucheza dansi ya twisti na roki en rol. Na wale wanawake wakijitupa wenyewe kwa kujinyonganyonga tu, wakiwa wameshikilia karatasi ya kijivu tu, ya kinafiki, ile … Kijivu iko kati ya nyeupe na nyeusi; ambayo ni rangi ya udanganyifu. Kijivu siyo nyeupe wala nyeusi. Ni rangi ya udanganyifu. Na karatasi inayoonekana ya kijivu, wakiwa wameishikilia mbele yao, wakiwa na sketi ya hula ya kuchezea dansi iliyo kama lesi ya nguo mbele yao, na wakiwa uchi kabisa kuanzia kiunoni kwenda juu. Na walikuwa wakitembea kwa … au wakati, au kujinyonganyonga, wakifanya mambo ya kipuuzi na ule muziki, wakitembea. Na kasema, "Hilo ndilo kanisa."

Na lilipopita pembeni mwangu, moyo wangu ulitaka kuzimia, Nikawaza, "Ikiwa kile ndicho kinachojaribu kupelekwa kwa Kristo kama Bibi arusi? Na juhudi yote na mambo ambayo mwanadamu ameyafanya, kujaribu kumleta Bibi arusi kwa ajili ya Kristo; na kahaba, mtovu wa adabu, mchafu, mwenye kutia kinyaa namna ile kuwa Bibi arusi wa Kristo?" Ilinifanya niugue moyoni mwangu.

23 Na alipokuwa akipita, baada ya … Akija mbele pale tuliposimama, alikuwa ameshikilia karatasi mbele yake, akijinyonganyonga, na kucheza dansi ya roki, na akienda upande mmoja halafu upande ule mwingine, alipokuwa akitembea, kama dansi za kisasa walizo nazo siku hizi akijifanyisha mwenyewe tendo la uasherati wakati akiwa anatembea.

Mimi siwajibiki na haya mambo. Naweza kusema tu kile nilichokiona. Na Mungu akiwa Hakimu wangu, lakini hilo lilikuwa kanisa la kutoka Marekani.

Sasa, alipokuwa akipita, sehemu yote ya nyuma haikuwa na nguo kabisa. Na ndipo alipokuwa akipita, nilijisikia kuzimia na kuugua.

Ndipo Yeye akasema, "Bibi arusi atakuja kuonyeshwa katika mwonekano wake wa awali tena." Na hapa akaja Bibi arusi nyuma yake, Bibi arusi yule yule aliyepita pale mwanzo. Ndipo moyo wangu ukaruka kwa furaha, kwa kujua kuwa kutakuwa na Bibi arusi. Na atakuwa amefanywa kwa jambo lile lile, na amevalishwa kwa kitu kile kile, kile kile alichokuwa amevaa Yule pale mwanzo. Inapasa Yeye aitwe. Na najua kuwa hiyo ndiyo Kweli. Ikiwa hilo sio kweli, basi kila ono ambalo nimekuwa nalo huko nyuma limekuwa makosa. Na kila mmoja anajua, kuwa hakuna jambo moja ambalo Yeye aliwahi kutuambia ila lile lilokuwa Kweli. Linakuja kutukia, vile tu …

Na je unaweza kuona, basi, ule uchafu wa kanisa la kisasa, likijiita lenyewe "kanisa"?

24 Kama mtu mmoja aliyesema siku ile; Ndugu Ruddell, ndugu yangu wa thamani, akiwa ameegemea ukuta pale sasa. Kwamba aliliona kama kimelea kwenye mzabibu. Na tulikuwa tunalijadili chumbani siku ile. Na Ndugu Ruddell alisumbuliwa moyoni kuhusu hali za wakati na-na hali ya kujisikia kiroho katika makanisa leo, jinsi ilivyoanza kushuka. Wachungaji wakija kutoka kila mahali, na mazungumzo nje hapa, wakiuliza, "Kumetokea nini, Ndugu Branham? Kumetokea nini?" Loo, jamani!

Ndugu Ruddell aliniuliza swali, "Je wanaishi kwa roho ya Shetani, au nini?"

Nikasema, "Hapana, kimelea huishi kwa nguvu ya mzabibu." Kinaishi kwa sababu, lile tunda la jamaa ya machungwa, mli-mlimao utakua kwenye mchungwa; lakini hautazaa machungwa, ingawa unaishi kwa uzima wake. Na, linaloitwa kanisa, ni chipukizi kimelea katika mti usio wake, likiishi chini ya jina la dini, chini ya jina la kanisa. Katoliki na Protestanti, ni vimelea tu, vikivuta … kutoka kwenye nguvu ya Mzabibu; na bado yakizaa matunda ya kile yalicho kwa sababu hawakuwa wameongoka. Hawakuwakatika asili, mpango wa Mungu wa tangu asili, hiyo ndiyo sababu inawapasa wakatae Neno na kuzaa aina nyingine za matunda. Mti halisi wa kweli, katika mzizi wake, ulichaguliwa tangu asili kuzaa machungwa kwenye mchungwa. Yesu alisema, "Mimi ni Mzabibu; nanyi ni matawi."

Lakini kama ule mti utakuja kamwe kutoa tawi lingine, hilo litazaa tunda lake la asili. Na ni lazima

pawepo na kurejeshwa kwa mambo haya yote, pale penye mwisho wa ule Mzabibu. Lazima pawepo, patokee kurejeshwa, Nuru ya jioni ya kuutia Huo nuru na kuufanya uwe sahihi. Lakini utatoka ndani ya Mzabibu, siyo dhehebu ambalo limepandikizwa kwake; bali ni uzao wa asili wa lile Neno. Inapasa ije kwa ajili ya wakati wa jioni. "Na kutakuweko Nuru wakati wa jioni." Inahitaji Nuru kuivisha Hilo.

25 Uone jinsi Andiko lilivyo kikamilifu! "Siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku." Tunda halitaiva isipokuwa jua liliivishe. Hata unahubiri kiasi gani, chochote ukifanyacho, halitaweza kuiva, halitaweza kudhihirishwa, halitaweza kuthibitishwa; ni kwa Yeye tu aliyesema, "Mimi ni Nuru ya ulimwengu," lile Neno. Hivyo yapasa ije nguvu, Roho Mtakatifu Mwenyewe, kuivisha, au kuthibitisha, au kuhakikisha, au kufanya dhahiri kile ambacho Yeye amekitabiri kuwa kingetukia katika siku hii. Nuru ya jioni huleta hilo. Ni wakati ulioje!

Bibi arusi alipita katika nafasi ile ile aliyokuwepo wakati alipokuwepo mwanzoni. Lakini nilikuwa ninamtazama wakati akijikanganya hatua za mwendo wake, na nikijaribu kumvuta arejee. Sasa, mengi yangeweza kusemwa juu ya mambo haya ya siku hii siku tunayoishi.

26 Sasa, Hosea alisema, katika 6:1 "Rudini Kwake Bwana." Kumbukeni, yeye alisema kuwa wangetawanywa, na ikawa hivyo. Yeye alisema, "Wao watamrudia Bwana, baada ya wao kutawanyika, na Yeye ange-atawatia upofu." Tazama, "Rudi … Tawanyika; ya pili … Wao waliraruliwa, na wakatiwa upofu." Hicho ndicho hasa kilichotuki. "Yeye atatuponya, na kutuganga jeraha zetu." Kama Ezekieli 37, "Mifupa mikavu, bonde lililojaa mifupa mikavu." Ezekieli aliliona hilo, kurejea kwao tena. Ndipo uone, Hosea alisema, "Baada ya siku mbili Yeye angerudi kwao. Yeye atatupokea na kutupa, atatuamsha sisi. Sasa, amsha haimaanishi "ufufuo." Amsha, pale, ni neno lile lile lililotumika mahali pengine popote, nililifuatilia hivi karibuni, linamaanisha "uamsho." "Yeye atatuamsha baada ya siku mbili." Hiyo ingekuwa "Katika siku ya tatu atatuamsha tena, baada ya kututawanya, na kutupofusha, na kuturarua."

Unajua, Wayahudi walipofushwa kwa ajili ya kusudi hilo kuwa sisi tupate kuona. Waliraruliwa vipande vipande, na kutawanywa, kama taifa, na wakamkataa Masihi wao; ili sisi tupate kumpokea Masihi, ili pawepo watu katika Mataifa watakaoitwa watoke nje, kwa ajili ya Jina Lake.

27 Sasa, mume anakuja, na mwanamke anachukua jina lake. Hawa Mataifa waliopofushwa macho, ambao hawawezi kuona lhilo Jina, "Bwana Yesu Kristo," katika ubatizo! Ni vibaya mno tu, lakini sharti iwe hivyo. Wayahudi ilipasa wae … Ilipasa wasilione hilo. Yupo mmoja tu awezaye kuliona hilo, huyo ndiye aliyekusudiwa tangu asili kuliona hilo. La sivyo hutaliona hilo kamwe. Wayahudi hawakuweza kumwona huyo kuwa Masihi wao. Na, bado, walikuwa wasomi na wanathilojia, watu wakuu wenye kisomo chenye hadhi ya juu, walisoma Biblia hii hii unayosoma. Sasa, baada ya hili kujulishwa kwetu, tumeliona hilo kwa uwazi, yule alikuwa Masihi. Lakini hawakuweza kuliona hilo, wala hawawezi kuliona leo. Wao wametabiriwa kuwa watapofushwa macho pia.

Kanisa siku hii, limetabiriwa kupofushwa, ili likatae Ujumbe wa wakati wa jioni. Ufunuo 3 lilisema hivyo, "Wewe mnyonge, mwenye mashaka," tazama hali ya bibi arusi usiku ule, au kanisa, "uchi, kipofu, nalo halijui." Bwana Yesu, turehemu! Biblia ilisema alikuwa "uchi." Sikuwahi kamwe kuliona hili hadi hivi punde tu sasa. Kanisa la Laodikia lilikuwa uchi. Na alipotokeza usiku ule, alikuwa "uchi," sikuwahi kuliona, "na sikulijua hilo."

28 Ee, ni shukrani iliyoje! Jinsi gani, ndio sababu tuna shukrani mno! Najisikia kuwa hatuna shukrani vya kutosha kwa ajili ya yale mambo ambayo Mungu anatufahamisha.

"Uchi." Na yale maono yalisema, yalinionyesha alikuwa uchi na hakujua, na "aliyepofushwa." Kama Israeli alivyopofushwa ili kwamba Mataifa waweze kuingia ndani, sasa Mataifa wamepofushwa ili kwamba Bibi arusi aweze kutolewa nje na Israeli waweze kupokea sikukuu ya Baragumu. Kamilifu tu!

"Baada ya siku mbili Yeye atatuamsha, au atatupa uamsho, akituleta pamoja, wale Wayahudi," nanena juu ya hizi Baragumu sasa. Na Yeye ata- … "Nasi tutaishi mbele Zake, au tuwe na Uzima wa Milele . Mnaona, tutakuwa mbele Zake." Biblia ilisema hapa katika Hosea, ikasema, "Nasi tutaishi mbele Zake; Uzima, tuwe na Uzima mbele Zake." Huo ni Uzima Wake Mwenyewe, Uzima wa Milele, "tuwe na Uzima mbele Zake." "Mke aishiye katika anasa amekufa akiwa bado anaishi." Kwa hiyo sisi … aliahidi kuwa Israeli angekuwa na Uzima mbele Zake tena. Yeye amekuwa mfu kwa mambo halisi ya kiroho na uhalisi wa sikukuuu ya Pentekoste.

29 Sasa tazama, kwa makini,:Ndipo baada ya siku mbili," sasa, hiyo haikumaanisha siku mbili za masaa ishirini na nne, kwa sababu kumekuwa na … Hilo lilitokea nyuma kule, miaka mamia mengi yaliyopita. Unaona? Lilimaansha, "siku mbili za Bwana," baada ya miaka elfu mbili. Sasa, mnajua umepita muda gani tangu wakati ule? Imekuwa miaka elfu mbili na mia saba tangu hilo, kwa sababu katika Hosea hapa ni mwaka 780 kabla ya Kristo. 1964, ona, imekuwa kitu zaidi ya miaka elfu mbili na mia saba iliyopita. Alisema, "Baada ya siku mbili, katika siku ya tata, Yeye atatuamsha tena, na kutupa Uzima mbele Zake." Hapo ndipo Baragumu zako zinaingia. Hiyo ndiyo saa tunayoishi, siku tunayoishi.

30 Sasa, wametawanywa, wamepofushwa, wamekusanywa, na wako ndani kabisa katika siku ya tatu. Mnaliona? Walitawanywa, kutoka Palestina, kwenda ulimwenguni kote. Walipofushwa, ili wamkatae Masihi. Na sasa wamekusanywa katika nchi yao, tayari kwa ajili ya Baragumu, ili watambue ule Upatanisho. Kama Biblia ilivyosema, "Watakapolipokea, na kumkuta Yeye akiwa na makovu ya misumari," baada ya Kanisa kuchukuliwa, "na waseme, 'Ulipata wapi haya makovu?' Akasema, 'Nyumbani mwa rafiki Zangu.'" Na Yeye akasema, "Watatengana, kila familia, na wangelia na kuomboleza, kwa siku nyingi, kama familia iliyompoteza mwana wao wa pekee." Kumbukeni, sikukuu ya Baragumu ilikuwa itende hilo. "kulia, kuomboleza kwa ajili ya Dhabihu iliyouawa," nao walikuwa wameikataa Hiyo.

Wako katika nchi yao. Walikuwa wametawanywa, wakapofushwa, na sasa wamekusanywa. Na lote lilikuwa chini ya ule Muhuri wa Sita, baragumu zao Saba … zilitoa sauti kuwakusanya pamoja, ile Baragumu ya Sita. Ile ya Saba ni "ile Baragumu Kuu," kama tulivyokuwa nayo Jumapili ilyopita. Ile Baragumu ya Sita ilitoa sauti chini ya Muhuri wa Sita. Kama tu Muhuri wetu wa Sita ulipofunguka, kila kitu kwa wakati ule ule; peke yake, zao zote zilitoa sauti kwa pamoja, ambapo tumekuwa miaka elfu mbili katika sikukuu ya Pentekoste.

31 Sasa, ni miaka elfu mbili na mia saba tangu wakati ule. Alisema, "Katika siku ya tatu, tutakusanyika tena. Baada ya siku mbili, katika siku ya tatu, tutakusanyika tena, na kupokea Uzima mbele Zake." Mnaona ahadi? Ile saa imeandikwa kikamilifu ukutani. Tunaona pale tunakoishi.

Sasa katika nchi yao ya nyumbani, wakisuburi sikukuu ya Baragumu, au kutambua Upatanisho, na kusubiri kule Kuja, kuomboleza kwa ajili ya kukataa kwao mara ya kwanza vile walivyolikataa Hili. Wako katika nchi yao ya nyumbani kwa ajili ya hilo, wakisubiri. Nini wote … Kila kitu kimewekwa mahali pake.

Nikiwa mhudumu wa Injili, sioni jambo lililobaki ila kuondoka kwa Bibi Aausi. Na Bibi arusi inabidi aondolewe kabla hawajatambua kile kilichotokea. Walikuwa wamefungwa, wametawanywa … Namaanisha, walitawanywawa wakapofushwa, na sasa wamekusanywa. Nini kimebaki? Yule Bibi arusi kuondolewa. Wanasubiri kuondoka kwa Bibi arusi, ili manabii wao wa Ufunuo 11 waweze kuwaingiza kwenye sikukuu ya Baragumu, kuwafanya watambue kile walichofanya.

32 Kumbukeni, pale pale katikati ya ile Mihuri, ulikuja Muhuri wa Sita. Na kulikuwa na mia moja na arobaini na nne elfu, waliochaguliwa na kuitwa. Na katikati ya Baragumu ya Sita na ya Saba, Ufunuo 11 inatokea pale pale hasa ukiendana na Muhuri wa Sita.

Ili kufanya nini? Ilikuwa ifanye nini? Na hii ilikuwa kuwaleta mashahidi wawili, Musa na Eliya, manabii. Kwani, Wayahudi huwaamini manabii wao pekee. Na wao watakuja na ishara ya manabii, na matendo yao yatakuwa yale ya nabii, kwani walifanya hivyo hivyo. Ikionyesha jambo moja, kuwa, binadamu unapokufa au chochote kile, unapoondoka katika huu ulimwengu, asili yako haibadiliki. Kama wewe ni mwongo sasa, utakuwa mwongo kule. Ikiwa wewe ni mkali hapa, utakuwa mkali kule. Wanaume na wanawake, ni wakati wa kujitikisatikisa wenyewe na kujichunguza wenyewe, na kuona pale tulikosimama, kwani kifo hakilibadilishi

33 Wamekuwa hawapo katika maisha haya kwa miaka elfu mbili. Musa karibu miaka elfu mbili na mia tano, na Eliya tangu hapo … Eliya amekwenda karibu miaka elfu mbili na mia tano, na Musa ameondoka, na wanarudi hapa na asili ile ile na kutenda mambo yale yale. Kifo hakimfanyi mtu lolote ila hubadilisha mahali pa kuishi. Hakibadilishi asili yako. Hakibadilishi imani yako. Hakibadilishi lolote ndani yako ila mahali pa kuishi.

Kwa hiyo, asili yako iko namna gani asubuhi hii! Ikiwa wewe unashuku Neno La Mungu, utashuku na kule. Sijali wewe ni mtakatifu jinsi gani, unaishi jinsi gani, na unaishi vizuri jinsi gani, kufa hakukubadilishi hata kidogo, ila mahali pako pa kuishi tu. Na ikiwa huwezi kulipokea Neno la Mungu lote jinsi lilivyoandikwa, hungelipokea lote Kule; hivyo usijali, hutakuweko Kule. Inakupasa kulipokea katika utimilifu Wake, katika nguvu ya kuthibitishwa Kwake na ufunuo wa kile lilicho, ndipo unakuwa sehemu Yake. Ni Neno Lake pekee ambalo Yeye atalifufua, kama Yeye alivyofanya Neno Lake kwenye asubuhi ya kwanza ya Pasaka. Neno lake pekee lilikuja, na wale waliokuwa wamekufa katika Neno lake, wakiamini Neno Lake na kuthibitisha Neno Lake.

34 Tazama, sasa, hilo limekuwa miaka elfu mbili na mia saba iliyopita. Tazama, walitawanywa, walipofushwa, na sasa wamekusanywa. Sasa, jambo linalofuata ni kwamba watapokea Uzima. [Ndugu Branham anagonga mimbarani-Mh.]

Na Mataifa wameitwa. Bibi arusi yuko tayari. Unyakuo uko karibu. Je, tunaweza kutambua hilo? Je, tunaweza kuamini hilo hasa? Ni hadithi iliyohadithiwa? Kwetu inaonekana ni habari iliyobuniwa? Ni kitu kinachoonekana halisi? Je, ni kitu ambacho sisi, nje, tunaweza kuamini? Au, ni kitu kilicho ndani yetu, ambacho ni sehemu yetu, kwamba ni zaidi ya uzima ndani yetu? Ni mtazamo gani tunaouweka katika hili, asubuhi hii, katika Hekalu hili? Kumbukeni, litakuwa kundi dogo litakalolipokea.

Sasa katika nchi ya nyumbani, wakisubiri zile Baragumu. Sasa wakisubiri kuondoka kwa Bibi arusi

mdogo, ili kwamba Ufunuo 11 uweze kutimizwa. Kipindi cha kanisa kimekoma; Mihuri imefunguliwa, ile iliyothibitisha kile walichobakiza katika kipindi cha kanisa, na Ujumbe umetolewa. Israeli ipo uwanjani, haleluya, tayari kwa ajili ya sikukuu ya Baragumu.

35 Ee, ninyi wanaume katika nchi nyingine mnakosikia hii kanda, hamwezi kuamka ndugu yangu? Au, inawapofusha? Je, mtalitupilia Hilo nje na kuliita unabii wa uongo? Wakati, linathibitishwa hapa hapa mbele yenu, na ulimwengu, na wakati, na watu, na Roho Mtakatifu Huyo aliyeliandika. Hilo limethibitishwa kwa hali zote, kiasili, kiroho na kwa mambo yanayoshikika. Kila jambo Yeye alilosema limetimizwa na kuthibitishwa.

Israeli nchini mwake; aliwapeleka mle, akawa mchungaji wao mle. Mbwa mwitu walimfuata na wakakimbilia kwenye usalama, kwenda kwenye nchi yao wenyewe. Kumbukeni Israeli, iliahidiwa kubarikiwa endapo ilikuwa nchini mwake. Mungu kamwe hakumbariki Israeli nje ya ile nchi. Abrahamu alikwenda nje ya nchi, akahukumiwa. Kila mmoja aachaye ile nchi anahukumiwa. Mungu anaweza kumbariki tu Israeli endapo anakaa katika nchi yake ya nyumbani, na yuko pale sasa kama taifa. Na Kanisa limeitwa; linasubiri tu Unyakuo, wa kumwondoa Bibi arusi.

Mihuri imefunguliwa. Imefunuliwa kwetu. Tunaone kile ilichokiacha. Ninyi mnaotaka kujadiliana na kuhangaika kuhusu uzao wa nyoka, na ubatizo wa maji, na kadhalika, mmepofushwa na hamna habari. Yule mungu wa ulimwengu huu amewapofusha, kwenye Hilo, nanyi hamna habari. Si ajabu nimekuwa na wakati kama huu asubuhi hii, nikipambana kuvunja na kupita katikati ya vikwazo!

Kwa hiyo manabii wao wataweza kudhihirishwa katika hii siku ya mwisho; hawawezi kulifanya; kwa Baragumu, ya sikukuu ya Baragumu.

36 Yeye alisema kupitia Hosea, "Nimekata." Sasa tazama, Yeye ananena na Israeli. "Nimekata," au kwa maneno mengine, "Nimekatakata, nimewakata vipande vipande, kupitia manabii." Hivyo ndivyo Mungu awatendavyo watu Wake. Aliwakatakata kutoka kwenye mataifa mengine yote. Kwa kitu gani? Upanga Wake ukatao kuwili, Neno lake. Aliwakatakata, taifa Lake, kutoka kwenye mataifa. Amekatakata taifa Lake kutoka kwenye mataifa, kwa kutumia manabii. Neno lake lililothibitishwa. Kwa hiyo amemkatakata Bibi arusi Wake kutoka kwenye madhehebu, kwa Neno lake; lililoahidiwa na Malaki 4, katika siku ya mwisho. Alimkatakata Bibi arusi Wake, alimkatakata kutoka kwenye makanisa! Alimkatakata Bibi arusi Wake!

37 Yeye, aliwakatakata Israeli kwa Neno Lake, lililowajia, kwa njia ya manabii Wake; "Jitengeni na hao wengine."

Angalia walipotaka kufanya kama wale wengine. Walikuja kwa nabii Samueli. Akasema, "Je, nimechukua fedha zenu? Niliwahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, ila lile lililotukia?

Wakasema, "Hapana, hiyo ni sahihi, ila bado tunanataka mfalme."

Hivyo ndivyo makanisa yalivyofanya. "Ee, tunaliamini Neno. Vema, lakini unajua, wanasema tungefanya hili." Sijali kile wanachosema. Neno liko sahihi!

Wakisubiri. Yeye amewakatakata, kupitia manabii.

Huu ni wakati gani ndugu? Ni wakati gani mhudumu? Mnaona wakati wa siku hii, na ishara mnayoishi chini yake? Mnaweza kulielewa? Mnaliona?

38 Kila mahali sasa, hakuna uamsho. Kila mtu analalamika, wahudumu wanalia. Nilikuwa nasoma mojawapo ya magazeti mashuhuri yanayokuja hapa kanisani, gazeti zuri sana. Na namfahamu mhariri, na nawafahamu wale watu na ni watu wacha Mungu, wazuri sana, Ndugu Na Dada Moore, wa Herald of His Coming. Moja ya magazeti mazuri zaidi yaliyo katika shamba la huduma, Herald of His Coming. Lakini watachapisha jambo lingine lolote kwa shida, isipokuwa, "Funga, omba! Funga, omba! Piga baragumu! Pata … Wangapi wanalisoma? Mnajua. Mnaliona wakati wote, "Funga, omba! Funga, omba!" Ni hayo tu mnasikia. "Funga, omba! Kuna siku kubwa tunayotazamia itachomoza! Kuna jambo kuu litakalotokea! Ninyi nyote, ombeni, ombeni, ombeni! Hatujachelewa mno bado!"

Kwani nini wanafanya hilo? Kwa nini wanafanya hilo? Wanahitaji uamsho mkuu. Wanalia, wakiamini kuwa kutakuwa na uamsho. Wao ni watu wazuri. Kwa nini ni hivyo? Wamefanya nini? Hawajatambua mwamko wa Bibi arusi. Unaona? Kule kuwa Mkristo, wanasikia mvuto wa wakati huu, ila hawajatambua kile kilichofanyika. Hilo ndilo linalowafanya wajisikie hivyo. Wanajua jambo fulani linapasa kutukia, lakini, unaona, wanalitazamia huko baadaye, lije, wakati tayari limekwishatukia pale pale ulipo.

Hilo ni jambo lile lile walilofanya siku za zamani. Walikuwa wanaamini kuja kwa Masihi. Waliamini kuwa kungekuwepo na mtangulizi atakayekuja. Lakini alikuwa pale pale mbele yao, na hawakulijua hilo. Hawakutambua hilo. Waliamini kungekuja mtangulizi ambaye angemtangulia Masihi, na wakamkata kichwa. Na wakamuua Masihi wao, kwa sababu ilitabiriwa kuwa wangepofushwa macho. Hosea alisema hivyo.

39 Na Roho yule yule aliyenena kupitia Hosea, alinena kupitia Yohana na kusema kanisa katika siku hizi za mwisho lingekuwa "uchi, na kipofu, na lingemfungia Yeye nje ya kanisa." Walishindwa kuona ule unabii ukitimia. Lakini, wakiwa pale, wanatambua kuwa jambo fulani inapasa litukie. Hawalielewi tu. Hawalitambui. Kama tu wale Wayahudi wa kale; Laodikia iliyopofushwa; utajiri, thilojia, wenye uhasama juu ya Kanisa, wenye uhasama juu ya Ujumbe. Tazama jinsi wale Wayahudi walivyokuwa na uhasama na Yohana. Tazama walivyokuwa na uhasama na Yesu, wakati Yeye alikuwa Yule Yule waliyedai kuwa wanamtafuta.

[Kile kifaa cha kukuzia sauti kinakoroma-Mh.] Naamini tumeunguza waya. Nadhani hilo linazima kinasa sauti pia. Halizimi. Vema.

40 Walikuwa na uhasama na Ujumbe.....

Kinachotokea ni kwamba, kuna harakati nyingi mno; kila mmoja wenu nyote ni kitu kimoja kinachotoa joto. Hakuna namna ya kuweka kanisa katika hali ya kawaida katika zile, chini ya zile nyakati. Kwa sababu unaona kila mmoja wenu ni BTU 98, kwa kawaida. Na hamkukaa pale namna hiyo tu; mnatoa joto daima. Kuna hewa ya kutosha humu ndani kuweza kupagandisha mahali hapa. Lakini, hiki kifaa cha kupasha joto kikiendelea kufanya kazi, hu-huwezi kufanya hilo.

Angalia, uhasama! Lakini, sasa, kama wale Wayahudi wa kale, walipofushwa! Wako kwenye Laodikia. Wako "uchi, wenye mashaka, maskini, na hawajui." Siku ya utajiri, mafundisho makuu ya thiolojia, elimu kuu, na sasa wamekuwa na uhasama na Ujumbe. Hawahitaji lolote juu Yake, kama tu ilivyokuwa huko nyuma kwenye siku Yesu wa Nazareti alipokuwa duniani.

41 Sababu watu, katika siku ya Nuhu, hawakuingia katika safina kwa sababu kamwe hawakutambua ujumbe wala yule mjumbe. Hiyo ndiyo sababu pekee wakaangamia, ni kwa sababu hawakutambua ile saa waliyokuwa wanaishi. Hawakutambua kuwa Mungu angeshughulika na dhambi kama Yeye alivyoahidi angefanya. "Angemwangamiza mwanadamu, atoke katika uso wa nchi." Yeye alitabiri hilo. Alilimaanisha. Na Yeye analimaanisha leo kama tu Yeye alivyofanya wakati ule.

Lakini watu, badala ya kuwa upande wa Nuhu, yeye alionekana mtu wa nyikani. Hawakumwamini yeye kuwa ni nabii. Unajua, Yesu, Yeye Mwenyewe, alituambia kuwa walidhihaki katika siku za Nuhu, walimdhihaki, wakamwita mshupavu wa dini na mengine mengi. Lakini hawakuitambua saa yao. Lakini hawakutambua ile ishara. Hawakutambua ule ujumbe. Hawakumtambua mjumbe, ila walimwondoa miongoni mwao na kumcheka. Yesu alisema, "Kama ilivokuwa katika siku za Nuhu."...."

42 Israeli akiwa nchini mwake, na kila kitu kikikaa mahali pake sasa, na Ujumbe ukiingia kwa ukamilifu tu, ni siku gani hii tunayoishi ndugu? Tuko wapi?

Hawakuijua ile siku. Hawakuijua. Hiyo ndiyo sababu waliikosa, ni kwa sababu hawakuitambua. Walikuwa katika siku ambayo ni kama watu walivyo leo, wamepofushwa na thibitisho za kisayansi, na mifumo ya elimu, na seminari za thiolojia. Na mambo yaliyowapofusha siku ile, yamefanya mambo yale yale leo. Yamewapofusha tena.

43 Na, vile vile, urahisi, urahisi wa ujumbe na mjumbe!

Nuhu hakuwa wa kisayansi. Hakuwa mtu msomi. Alikuwa mkulima maskini, mnyenyekevu, akiwa na ujumbe mrahisi. Ulikwa mrahisi mno kulingana na elimu yao ya juu. Ndivyo ilivyo leo. Mungu siku zote huufanya mrahisi, ili apate watu watakaomwamini na kumtumainia Yeye. Ni tofauti, Ujumbe tofauti tu, lakini Mungu yule yule. Sasa nataka ninyi muamini Huo na kuelewa kuwa Mungu ameunena Huo.

Yesu alisema walimdhihaki nabii Wake, Nuhu. Na kama walivyodhihaki siku ile, ndivyo watakavyofanya tena kwenye Kuja Kwake. Watafanya jambo lile lile. Hiyo ndiyo sababu yule Farao alizama baharini. Kamwe hakuitambua siku yake. Kamwe hakutambua kile kilichokuwa kinaendelea. Alivutiwa zaidi na mafanikio ya kipindi chake cha sayansi, kujenga miji kwa kazi ya watumwa. Alikuwa-alikuwa na shughuli nyingi mno, hata asiweze kutambua nafasi aliyokuwa nayo, na akamfukuza mjumbe-nabii wa Mungu kwenda jangwani. Yeye hakuitambua. Hiyo ndiyo sababu kwamba mambo yalikwenda hivyo. Kamwe yeye hakuitambua. Laiti angeweza kutambua lile Neno la Mungu lililoahidiwa kwa ajili ya wale watu!

44 Na kama makanisa leo yangetambua tu, ikiwa makansa yangetambua tu Neno la Mungu ambalo limefanya hii ahadi kwa ajili ya saa hii, kwa ajili ya watu, wasingeliangamia. Ikiwa Marekani wangeweza tu kutambua ile katiba aliyoiweka, hangekubali kuondoa Biblia mashuleni, kuondoa Jina la Mungu toka kwenye sarafu, na aahidi utiifu kwa Mungu. Lakini hatambui hilo. Kwa nini? Yeye ni kipofu, yu uchi. Hawezi kuitambua damu ya wale wavulana wa thamani waliokufa kwenye mapigano kwa ajili ya hii tunu. Wamesahaulika; wao ni mavumbi.

45 Lakini kuna Mmoja Ambaye anakumbuka kumwagika kwa damu ya manabii, gharama iliyochukua kuileta hii Injili kwetu leo. Jinsi maelfu walivyoliwa na simba, na kutupwa kwenye matundu ya wanyama, waliokatwa na kutenganishwa kwa msumeno, waliochomwa moto, waliosulubishwa! Mungu analitambua

hilo. Kanisa limewasahau manabii wao. Wanadai wao "hawawahitaji tena." Lakini Mungu anajua inampasa kuwa nao; Yeye huwakatakata watu Wake kwa Neno Lake. Lakini ni la kizamani mno kwao katika siku hii. Hawalitambui Hilo. Ndiyo sababu wako katika hali waliyoko sasa. Hiyo ndiyo sababu wako "uchi, maskini, vipofu, mnyonge, na hawajui," kwa sababu hawaitambui ile saa wanayoishi. Hawaioni.

46 Musa, yeye aliitambua siku yake na wito wake, alipoona ile ahadi ya Neno la Mungu kwa ajili ya ile siku ikithibitishwa. Alijua basi, na kutambua yeye alikuwa nani na alikuwa afanye nini, kwa Neno lililoahidiwa. Kwa hiyo hakuogopa chochote alichosema mtu yeyote. Hakuuonea ujumbe wake haya, ingawa kila kasisi na kila Farao, kila kitu, kila mamlaka hayakukubaliana naye. Lakini yeye alitambua alipoiona ile Nuru, ile Nguzo ya Moto ikining'inia katika kile kichaka, na kunena naye lile Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku ile, na kusema, "Nimekuita kwenda kufanya hilo." Hakuogopa yale-yale matisho makuu ya mfalme. Alikwenda kuwaleta wale watu kwenye kutoka, kama Neno la Mungu lilivyokwishaahidi.

47 Alipoona ile ahadi ikithibitishwa, yeye aliwaweka watu wawe tayari kwa ajili ya kutoka kwao. Lini? Wakati alipoona ahadi ya Mungu ikithibitishwa. Kumbukeni, yeye alikimbia na thiolojia yake; alikimbia na mafunzo yake. Lakini alipoona Neno la Mungu likidhihirishwa, aliona likithibitishwa, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO," basi hakujali yeyote alichosema. Hakuogopa kile Farao angefanya naye. Hakuogopa kile wale wengine wangefanya. Alimwogopa Mungu pekee, kwamba angeweza kutomwelewa Mungu, au kwa namna fulani angeweza kutomwelewa Mungu. Hakuogopa wale watu na kile wangesema au kile wangefanya. Alimwogopa Mungu pekee, baada ya yeye kutambua lilikuwa Neno la Mungu.

48 Yeye hakuweza kuelewa jinsi mtu kama yeye angepelekwa chini kule. Lakini alipotambua, kwa Neno lililothibitishwa, ilikuwa nini, basi hakuogopa amri za mfalme. Kama tu ungetambua, kama sisi tungeweza tu kutambua leo! Musa alilitambua alipoona Neno likithibitishwa, aliona uthibitisho ukihakikishwa, yeye alikuwa tayari kwa ajili ya kutoka kwa wale watu. Ayubu kamwe hakutambua kwamba ilikuwa ni Mungu. Maadam shetani anaweza-anaweza kukufanya uamini wakati mwingine kuwa majaribu madogo unayopitia ni-ni Mungu anaweza … anakuadhibu! Ilikuwa Mungu akijaribu kumwonyesha kitu fulani. Ayubu kamwe hakulitambua hadi alipoona ono. Kama Musa; Musa alipoona ono, ile Nguzo ya Moto kichakani, hilo lilithibitishwa. Na wakati … Ayubu, katika swali lake, "Mtu akifa, je atakuwa hai tena? Naona mti ukifa, na utachipuka tena. Naona ua likifa, na linaishi tena." Hilo lilikuwa swali lake. "Lakini mwanadamu hulala chini, hutoa roho yake, anapotelea mbali. Wanawe huja na kuomboleza, wala yeye hajui. Ee, laiti ungenificha kuzimuni hata ghadhabu zako zitakapopita!" Hakuelewa kwa nini ua lingekufa na kuwa hai tena kwa jinsi jani lingeanguka kutoka kwenye mti, chini, na kulala ardhini, na kurudi tena katika kipindi cha kuchipua. Alisema, "Mwanadamu hulala chini, naye anakwenda wapi? Namwamini Mungu; lakini nini hutokea kwa mwanadamu?"

Lakini ndipo siku moja kimulimuli kikaanza kumulika, ngurumo zikaanza kunguruma, Roho akaja juu ya nabii. Na yeye akaona kuja kwa Mtu Ambaye angeweza kuweka mkono Wake juu ya mwanadamu mwenye dhambi, na Mungu mtakatifu, na kuweka daraja. Ndipo akapiga yowe, "Najua Mkombozi wangu yu hai! Ijapokuwa mabuu yataharibu mwili huu, bado katika mwili huu nitamwona Mungu!" Yeye alitambua ufufuo ulikuwa nini.

49 Balaamu kamwe hakumtambua yule Malaika hadi punda aliponena kwa lugha. Balaamu hangeweza kutambua kuwa yule Malaika alikuwa amesimama mbele yake. Mhubiri aliyepofushwa hangeweza kutambua kuwa ilikuwa Mungu amesimama njiani, akijaribu kumzuia asiuze karama yake kwa ajili ya kupata fedha. Na yule punda aliponena katika sauti ya mwanadamu, ndipo Balaamu akatambua kuwa alikuwa Malaika akiwa amesimama njiani, akijaribu kumzuia asifanye kile alichokuwa anafanya.

Ee, enyi madhehebu mliopofushwa! Ikiwa Mungu anaweza kumtumia punda, ambaye ni bubu, anene kwa lugha asiyoijua, kufunua kwa mhudumu kuwa ameiacha njia, je hawezi kumtumia mwanadamu kufanya jambo lile lile? Watu waliopofushwa!

50 Ikiwa Ahabu angetambua siku yake, kamwe hangemshutumu yule nabii, Mikaya, aliyekuwa na Neno la ahadi la Mungu kwa ajili yake.

Ahabu aliposimama pale siku ile, yeye na-na Yehoshafati. Na walipokuwa na manabii mia nne kule wakitabiri, wakisema, "Kwea! Kila kitu kiko sawa. Ahabu, unaishi katika dhambi. Umetufanya dhehebu kuu! Sisi ni watu mashuhuri. Sisi ni shirika kuu la dini. Tuko hapa, sisi ni makuhani mia nne waliofuzu, au manabii. Sisi ni mia nne tuliofundishwa katika Neno na thiolojia. Tunajua yote kuhusu Hilo."

Kwa hiyo, sasa, hiyo ilithibitisha kuwa hawakujua yote kuhusu Hilo. Yule mtu waliyemwita kichaa, katika kizazi kabla yao, Eliya, nabii wa kweli wa Mungu, alikuwa ametabiri "HIVI ASEMA BWANA, 'Mbwa wataramba damu yako Ahabu!'" Unaona?

Lakini wale makuhani, manabii waliowekwa na wanadamu, walifikiri walikwishapanga kila kitu na kingekwenda hivyo tu.. Walisema, "Baba Abrahamu … au, Baba Ahabu, kwea! Bwana yuko pamoja nawe. Unayo Maandiko, kwa sababu Mungu aliwapa Israeli hii nchi. Ni ya Israeli. Kwea! Bwana yuko pamoja nawe." Loo, jamani!

51 Lakini, unajua, Yehoshafati, yule ambaye hakuwa amejichanganya katika dhambi kama Ahabu alivyofanya, aliona mambo tofauti kidogo. Akasema, "Hakuna mwingine?"

Akasema, "Tunaye mmoja hapa, lakini namchukia." Unaona? Mungu alikuwa anafanya nini? Anawakatakata watu wake kwa kutumia nabii, tena. "Namchukia huyu. Yeye hafanyi chochote isipokuwa kunihukumu mimi wakati wote. Na unajua kuwa mimi ni mtu mkuu. Nisingekuwa na hii seminari chini hapa kama nisingekuwa mwamini mkuu. Ninao watu waliofuzu vema katika taaluma. Nimewaweka chini pale pamoja na vitabu na Biblia, na kila kitu kinginecho, ili kufundisha hili. Na ninajua ni watu wakuu." Lakini kama Ahabu angelikuwa ametambua tu kuwa yule jamaa alikuwa ni nani, huyu mtu maskini aliyevaa nguo za ovyo, mwana wa Imla, akiwa amesimama pale, akimwambia, "HIVI ASEMA BWANA," asingekuwa amefanya kosa hilo kubwa alilolifanya. Lakini yeye alimhukumu Mikaya. Yeye kamwe haku …

Ee, watu, tambueni kipindi ambacho mnaishi! Tazameni yalikwishatokea. Tazameni yaliyoahidiwa. Tambueni siku mnayoishi.

52 Ikiwa kanisa la kidhehebu leo lingeweza kutambua tu kwa nini wanashutumiwa, na washirika wao wanakimbia kutoka kwao, kama Israeli walivyotoka Misri! Kama madhehebu yangeacha kushutumu zile kanda, na wazisikilize! Na wewe, mhubiri, unayesikiliza hii kanda, sikiliza! Kama tu ungetambua tu ile saa unayoishi, kama tu ungetambua ile ishara ya wakati, ungeona ni kwa nini watu wanakimbia kutoka kwenye madhehebu. Roho wa Bwana akiita! Yesu alisema "Hakuna mtu ajaye Kwangu ," "isipokuwa amevutwa na Baba Yangu. Na wote Baba alio nao, katika nyakati zilizopita, alionipa Mimi, watakuja."

53 Kama yule mwanamke mdogo pale kisimani, na kuhani, walitofautiana jinsi gani! Yale maandiko yako kwenye ukuta wa leo tena. Wanayaona lakini hawayatambui.

Kama Wayahudi wangekuwa wametambua tu ile ishara iliyoahidiwa ya Masihi wao, kulingana na nabii wao wa mwisho! Malaki 3 ilisema. "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele za uso Wangu, naye atatayarisha njia." Na walidai wao walikuwa wanamtafuta. Ni-ni sambamba vipi, hadi le-leo!

Wanadai wanatazamia jambo fulani litokee. Makanisa yote yanaomba na kufunga, na kusema, "Sasa hebu tuombe. Hebu tuwe pamoja. Inatupasa tuwe na jambo kuu litakalotokea. Tunajua kuna jambo kuu litatokea. Lile Kanisa yapasa liwe tayari." Hilo ndilo wao wanaloombea.

54 Hilo ndilo walilokuwa wakiombea kule. Na pale akaja Yohana Mbatizaji. Kwa kuwa yeye alikataa seminari zao za dini, kwa sababu alifanya kinyume na kile baba zao walichofundisha. Akatoka nyikani bila elimu. Akatoka bila ukosi uliogeuzwa, kama ambavyo ingesemwa leo. Alitoka bila thiolojia kubwa. Lakini alikuja, akijua kwa ahadi ya Mungu kuwa yeye alikuwa amtangaze Masihi. Akasema, "Yeye amesimama miongoni mwenu." Nao walidhani alikuwa mwendawazimu, kwa sababu hakutoka kwenye mashule yao. Maandiko yalikuwa ukutani, na hawakujua. Walidai walikuwa wanamtazamia Mtu kama huyu aje; na Yeye alikuwa pale pale miongoni mwao. Nao hawakumtambua, ingawa walisema walikuwa wanamtafuta Yeye.

55 Linafanana tu, kama Wayahudi, wao wako ndani, ndivyo hivyo pia Mataifa kwa upande, kwa sababu ilitabiriwa jambo lile lile, jambo lile lile. Walidai kuwa walikuwa wanamtafuta Yeye. Lakini madhehebu sasa katika Mataifa, kipindi cha Laodikia ni vipofu tu kama hao walivyokuwa, kwa sababu (kwa nini?) ilitabiriwa wangekuwa hivyo. Lazima litukie.

Ikiwa Israeli wangeweza tu kutambua ishara yao, wangejua wakati wa kutokea kwa Masihi ulikuwa umetimia. Kama wangetambua!

Unajua wale-wale wanafunzi walisema hilo kwa Yesu. "Mbona waandishi husema, kuwa 'Eliya yu aja kwanza?'"

Na Yesu akasema, "Eliya tayari amekuja, na hawakumjua. Ameshakuwa hapa, na tayari wamekwishamuua. Walitenda kile hasa Maandiko yalichosema wangalitenda."

56 Kama wangelikuwa wametambua hilo tu, yule "mshupavu wa dini" yule aliyeshutumu kila mambo ya hila waliyofanya, yule aliyeshutumu kila kitu walichokuwa wakifanya! Akasema, "Enyi wanafiki! Msianze ku- … Nyoka kwenye majani, enyi kizazi cha nyoka, nani amewaonya kuikimbia ghadhabu itakayokuja? Msianze kuwaza ndani mwenu, 'Tunaye Abrahamu akiwa Baba yetu. Tuna hiki, au kingine! Kwani nawaambia, Mungu anaweza kumwinulia Abrahamu watoto kutoka kwenye haya mawe."

Msianze kuwaza kuwa mnalo Baraza la Ulimwengu mikononi mwenu, na mnao washirika waliovaa vizuri kuliko wengine wote. Mungu anaweza kuinua watoto kutokana na mapanya wa vichakani ili kutimiza Neno Lake; makahaba, wazururaji, walevi, wacheza kamari. Yeye anaweza kufanya hilo. Yeye bado ni Mungu.

57 Madhehebu yaliyopofushwa, kama Israeli iliyopofushwa, yote yalitabiriwa kuwa hivyo. Nawaonyesha ulinganifu, hadi nifike kwenye hii sehemu ninayotaka sasa. Waliopofushwa, kama yale-yale madhehebu ya Mataifa ya Kipindi cha Laodikia yaliyopofushwa leo kama walivyokuwa wakati ule.

Kipindi cha Laodikia kinapaswa kupokea Ujumbe! Malaki 4 ilisema kingepokea. Lakini wanatafuta nini?

"Dhehebu letu litatengeneza Hilo. Ikiwa haliji kupitia sisi, Baptist, Presibiteri, Assemblies, Oneness, au kitu fulani, naam, ikiwa hatuliundi Hilo sisi, Hilo si kweli." Jambo lile lile walilofanya siku ile! Na lilikuja na kupita, na hawakujua. Hawakulitambua, ingawa lilitimiza kila neno. Yesu alisema, "Wamefanya kama ilivyokuwa imeorodheshwa kuwa wangefanya. Vivyo hivyo watamtenda Mwana wa Adamu; yeye atakataliwa.

58 Sasa tazama, ni jambo lile lile sasa katika siku za Mataifa, kufuatana na Maandiko yaliyoahidiwa ya Malaki 4. Ambapo, Yesu alisema, "Kila Andiko limevuviwa, na hakuna hata sehemu moja yake ambayo haitatimia." Hakuna njia yoyote ya kufanya Andiko lisitimie. Yote lazima yatimizwe. Na Yesu alisema lingetokea. Na hapa tunaona limetokea. Tunaliona.

"Kurejesha" nini, katika siku hizi za mwisho? Enyi ndugu wa kidhehebu, sikilizeni! Rejesheni ile pentekoste, sikukuu ya asili. Kama ilivyokuwa hapo mwanzo, ndivyo itakavyorejeshwa kabla Baragumu ya sikukuu ya Israeli haijatoa sauti. Inapasa irejeshwe! Lazima kuwe na jambo la kuifanya hiyo. Malaki 4 ilisema ingerejeshwa. Imani ya baba, kwa watoto, kile ambacho kingetukia.

Ikiwa Israeli ingemtambua Masihi wao, ishara iliyoahidiwa, wasingekuwa hapa walipo leo. Kama wange … Lakini ni kwa nini hawakufanya hilo? Inatia huruma. Kwa nini hawakufanya hilo? Kwa sababu Mungu alisema wasingefanya hilo. Wangapi wanaamini hilo, semeni, "Amina." [Kusanyiko sasa linasema, "Amina!"-Mh.] Mungu alisema wasingefanya hilo. Na ni jambo lile lile Mungu amesema, katika Kipindi cha Kanisa la Laodikia, hili lingetokea, na hili hapa mbele yao. Wanawezaje kufanya jambo lolote ila kufanya hilo?

59 Ikiwa tu wangetambua ile ishara iliyoahidiwa ya Masihi, ile ishara ya Mwana wa Adamu! Yeye alikuja kwa jina la Mwana wa Adamu. Sasa, Yeye alikuwa katika jina, kupitia Kipindi cha Pentekoste, katika Roho Mtakatifu, Mwana wa Mungu. Sasa, jambo linalofuata ni Utawala wa Miaka Elfu, Mwana wa Daudi. "Wana" watatu, Mungu yule yule. Yule yule, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," Mungu yule yule. Mwana wa Daudi, Mwana wa Mungu … Mwana wa Daudi, Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, katika Mungu yule yule wakati wote, katika kazi tatu tofauti za ofisi.

Kwa hiyo ni "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" sio Mungu watatu, ila Mungu yule yule katika vipindi vitatu, kazi tatu, kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Lakini, kama leo hii, wamepofushwa na mapokeo kama walivyokuwa wakati ule, wamepofushwa kwa mapokeo, hawalioni. Kwa nini hawawezi kuliona? Kamwe hawataliona. Kumbukeni, hiyo ni HIVI ASEMA BWANA. Unasema, "Kwa nini basi unasema hilo?" Kama tu vile alivyofanya Yohana, lile lile kama walivyofanya wale wengine. Kuna moja limenata hapa na pale, linalopasa liletwe. Ee, kondoo wa Mungu, sikieni Sauti ya Mungu! "Kondoo wangu huisikia Sauti Yangu."

60 Yule mwanamke pale kisimani alitambua siku yake kwa ishara ya Masihi. Alikuwa katika hali mbaya. Hakutaka kujipumbaza na yale makanisa ya zamani, jinsi yalivyokuwa yanafanya. Yalikuwa yanaishi vyovyote, na yale mambo waliyokuwa yanayafanya, hakuyaamini hayo. Lakini alijua kungekuja Mmoja siku moja. Yule mtu masikini juu kule, akielekea kisimani; alipata lile Jambo alilokuwa analitafuta, wakati yeye alipoanza kumfunulia siri ya moyo wake, akamwambia dhambi aliyokuwa anaishi ndani yake. Akasema, "Bwana, naona kuwa Wewe ni Nabii." Sasa, hawakuwa na mmoja kwa miaka mia nne. Akasema, "Naona kuwa Wewe ni Nabii. Na najua kuwa Masihi atakapokuja Yeye atafanya haya mambo."

Akasema, "Mimi Ndiye."

Akatambua. Hakukuwa na maswali zaidi, "Unawezaje kulithibitisha?" Lilikuwa tayari limethibitishwa. "Masihi atakapokuja, hilo ndilo Yeye atafanya." [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara tano-Mh.] Vema, iwapo anaweza kulitambua kwa Maandiko, je sisi hatuwezi kutambua Nuru za jioni na ile ishara ya leo? "Tunajua Masihi ajapo Yeye atatuonyesha haya mambo yote. Yeye atatuambia hili."

Akasema, "Mimi Ndiye anayenena nawe."

Hakuna maswali zaidi. Akaondoka, na kuwaambia watu, "Njoni, angalieni! Yuko hapa." Hakuna swali zaidi kwake. Lilikwisha, kwa sababu alitambua ile siku aliyokuwa anaishi ndani yake. Aliitambua.

61 Hivyo hivyo na Nathanaeli, Mwebrania mkuu, yeye alipoiona ile ishara ya Masihi iliyoahidiwa pale; haidhuru ni makuhani wangapi, ni vitu vingine vingapi. Ilifanya nini? Iliwasumbua makuhani, kuona wale watu wakiondoka makanisani na kwenda zao. Akasema, "Kama yeyote kati yenu akihudhuria mkutano Wake, atatengwa. Tutakutoa dhehebuni pale pale."

Ndivyo ilivyo leo. "Tutakutoa kwenye shirika letu kama utahudhuria mkutano wake."

Mnamkumbuka yule mtu kipofu? Baba na mama hawakuweza hata kujibu; walikuwa wameogopa. Kwa sababu, walisema, "Mtu yeyote aliyekwenda kwa Yesu, au-au aliyehudhuria mikutano Yake, watatengwa." Lakini yule mtu kipofu aliweza kujisemea mwenyewe, yeye aliyekuwa kipofu akawa ameweza kuona.

Mimi, niliyekuwa kipofu hapo mwanzo, naweza sasa kuona. Mimi, ambaye sikujua haya mambo, nimejulishwa Hilo na Roho Mtakatifu. Fungukeni, madhehebu, kwa sababu wanakuja, vyovyote vile!

"Kama nikichukuliwa juu kutoka duniani, nitawavuta wote Kwangu."

62 Nathanaeli alilitambua hilo. Alilijua hilo.

Kama tu Maandiko ya Musa yanavyothibitisha, yalivyolithibitisha Neno. Musa alijua kuwa ile ilikuwa ahadi ya ile siku, kwa sababu lilikuwa la Kimaandiko, haidhuru ni la kigeni jinsi gani. Akasema, "Nani atakayewaambia … Nitawaambia niliona Nuru nyuma hapa nyikani. Nitawaambiaje sasa kuwa kulikuwa na Nuru hapa, na hii Nuru iliniambia niende chini kule?"

Yeye Akasema, "Hakika, Musa, nitakuwa pamoja nawe." Na sio tu … Yeye hakujionyesha mwenyewe kule Misri; ila kwa miujiza na ishara pekee. Lakini Yeye alipowakusanya wote pamoja, aliwatokea tena, na kuthibitisha huduma ya Musa mbele ya Wateule na walioitwa. Yule nabii alipokuwa amewakatakata na kuwafungua kutoka lile taifa na kuwaleta hadi mahali, ndipo ile Nguzo ya Moto ikawatokea tena, na juu ya Mlima Sinai.

63 Lilinganishe na leo. Amina! Utukufu kwa Mungu! Ni zaidi ya uzima kwangu.

Na umri wangu unaanza kujikongoja, na naona saa ya uharibifu wa maadili na tabia mbaya za kiasherati ikifagia nchi na vitu kama hivyo, ndipo natazama nyuma na kuona kile kilichotokea. Moyo wangu unaruka kwa furaha, nikijua kuwa baada ya muda mfupi hili hekalu la makazi la kidunia litakwisha, lakini nina moja linalosubiri kule. Ninajaribu kuwavuta watu, kuwakatakata kutoka kwenye haya mambo na vitu vya aina hiyo, kuwavuta nje; kuwaonyesha, kwa Maandiko, kuwa Mungu amesimama pale; akiwa na uthibitisho wa Nguzo ya Moto, ambayo mamia na maelfu wameiona, na hata wameipiga picha, hapo kabla, kwa kamera, wakati baada ya wakati, kulithibitisha.

64 Waigizaji huinuka. Hakika, lazima lifanyike. Waigizaji waliinuka katika siku ya Musa na kufanya jambo lile lile. Mungu alisema, "Jitenge mwenyewe Musa. Usikae karibu nao. Nitawameza." Na ulimwengu ukawameza. Na ni vivyo hivyo leo; kurudi moja kwa moja ulimwenguni, mipango ya fedha na kila kitu kingine. Unaona?

Ishara ya Kimaandiko ya Musa! Yeye alikuwa-yeye alikuwa yule nabii mkuu wa Mungu aliyekwenda chini kule kuwakomboa, nao wakalitambua hilo. Waliitambua ile ishara. Yeye alikuwa ahadi kamili ya Maandiko iliyothibitishwa.

Yesu alikuwa ile ahadi ya Maandiko, iliyothibitishwa kwa yule mwanamke. Au, Yeye alikuwa Fasiri. Yesu alikuwa Fasiri ya Maandiko. Maisha Yake Mwenyewe yalifasiri Maandiko.

Je, huoni Ujumbe wa saa hii? Unaweza kutambua mahali tulipo? Ujumbe wenyewe, kutoka kwenye Maandiko, unakufasiria ile saa tunayoishi. Hiyo ni fasiri.

65 Yesu aliwaambia Israeli, "Kama tu ungejua siku yako." Wakati mmoja, akiwa ameketi juu ya Mlima wa Mizeituni, alitazama, akasema, "Yerusalemu, Ee Yerusalemu!" Akalia. Akatazama chini. Akaona. Siyo kwa ulinganisho wowote labda. Usiku ule mwingine, asubuhi ile, kwenye saa nne, nilipoona lile kanisa kahaba. Kwenye kilindi cha moyo wako, unamsikia Roho Mtakatifu akidondosha machozi. "Yerusalemu, Eee Yerusalemu mara ngapi nitakufunika. Lakini ulifanya nini? Uliwaua manabii niliowatuma kwako. Uliwaua." Na Jumbe zimetumwa kwa kanisa leo, zimeuawa na imani zilizotungwa za kidhehebu. Maandiko yameuawa na imani hizo imani zao. Yesu alisema, "Kama ungeijua tu siku yako! Lakini, ni mbali mno sasa, mmechelewa mno sasa." Ndivyo ilivyo kwa makanisa!

Ninaamini, kwa moyo wangu wote, kanisa limekwishavuka ukombozi. Haidhuru ni nini unataka kufikiri kuhusu hilo, ni maoni yako peke yako. Hili ni langu. Unaona? Hulazimiki kuwa na maoni yangu. Lakini naamini limekwishavuka upeo wa ukombozi, na ni tangu miaka mitano au sita iliyopita. Nakumbuka. Mnakumbuka Chicago. Tazama kile kilichotokea tangu wakati ule, na kione kikiendelea kutokea. Unaona? Kumbukeni, jina langu liko mbele yake. Limebandikwa nje kule. Ni HIVI ASEMA BWANA. Angalia kama halijadondoka, endelea.

66 Tazama kwenye mwaka 1933, jinsi lilivyosema wanawake wangefanya katika hizi siku za mwisho. Jinsi lilivyosema watu … Jinsi Mussolini, jinsi ambavyo angefikia mwisho wake. Jinsi Hitler angekuja kwenye mwisho wa kimafumbo. Jinsi zile itikadi tatu za kisiasa zingeishia kwenye Ukomunisti. Jinsi kwamba mitambo ingekuja yenye umbo la yai. Na jinsi kwamba wanawake wangevaa mavazi na kuonekana kama wanaume kama nguo zao za ndani vile vile; na mwishoni wangeweka kama majani ya mtini, juu yao. Ni tendo la kiasherati jinsi gani jinsi ambavyo wangetenda katika siku hii. Tazama yale ambayo wamekwishatenda. Na lipo pale pale mbele yako basi.

Ikiwa wanawake wa Kikristo wangeweza tu … wale wanaoitwa wanawake Wakristo wangetambua tu, wangetambua kuwa hiyo roho ya uovu iliyoko juu yao ni ya Ibilisi, kuwafanya wakate nywele zao. Ibilisi

ndicho kitu pekee kingefanya hilo. Hilo ni kinyume na Neno la Mungu kwako, kama tu ilivyokuwa katika bustani ya Edeni. Walifanya nini? Laiti wangelitambua! Wanajaribu kusema, "Ee, yule mhubiri mzee mdogo anayejifanya mtakatifu anayejiviringisha, akisema, "Sio mimi. Siwaambii kile cha kufanya. Nanukuu Neno tu. Laiti wangelitambua kuwa huyo ni Shetani.

67 Wanajiita wenyewe Wakristo. Yesu alisema, "Mnawezaje kuniita, 'Bwana,' na msifanye mambo yale niwaambiayo mfanye?" Hawawezi kuwa Wakristo! Mimi sio hakimu wao, ila nasema tu kile Neno lilichosema. "Mnawezaje kuniita, 'Bwana,' na msifanye yale mambo niliyosema mfanye?" Na Neno lote hapa ni ufunuo wa Yesu Kristo. "Mnawezaje kuniita, 'Bwana,?"

Laiti wangelitambua ni Ibilisi, roho ya uovu. Wanawake fulani wazuri kule …

Nadhani hapa ni mahali penye utovu wa adabu kuliko kote nilikowahi kuona katika maisha yangu, Jeffersonville, Indiana, kwa wanawake walio uchi. Nimekwishawahi kuwa kule Hollywood. Nimekwishakuwa kila mahali. Nimekwishakuwa kote ulimwenguni, na nimeona namna zote za uchafu. Nimekwishaona kule Paris. Nimekwishauona Uingereza, ambayo ndiyo mkuu wa hao wengine wote.

68 Nadhani kuwa Uingereza ingezama siku moja chini ya bahari. Inastahili hilo; kinyaa, mazungumzo machafu, udhaifu! Hilo ndilo jalala la maovu la ulimwengu, watu waliopotoka na wakanaji wa Maandiko zaidi ya wote niliowahi kuwaona katika maisha yangu. Uingereza imekuwa hivyo kwa sababu imeikataa ile Kweli.

Billy Graham alisema ilimlazimu kumwondoa mke wake kutoka kwenye viwanja vya mapumziko; mambo ya ngono yaliyokuwa yanaendelea kati ya wanaume na wanawake, wavulana na wasichana pale pale kwenye viwanja vya mapumziko, katika uwazi. Uingereza imekuwa jalala la la maovu; vivyo hivyo na Ufaransa, vivyo hivyo ulimwengu uliobaki wote. Na vivyo hivyo Marekani, ikiwa kiongozi wa wote!

Tazama leo. Huwafanya wakate nywele zao, wavae kaptula, visketi vifupi sana, wavute sigara, na kujiita waamini. Je, hutambui dada, au mwanamke … Namaanisha, samahani, siyo dada yangu; hufanya jambo kama hilo. Hamtambui kuwa ni Ibilisi? Lakini kile … Kama wale Wayahudi wa kale, hamtaamini Neno lililothibitishwa linapothibitishwa kwenu. Mnang'ang'ania pale pale kwenye mila zenu za kidhehebu zinazosema mambo yote ni sahihi. Mnanena kwa lugha, mnarukaruka juu-na-chini, mnaimba katika roho, na mnakata nywele zenu. Mnaweza kuwazia Mkristo akifanya hilo? Nimewaona mapepo, nimewaona wachawi, nimewaona wakinena kwa lugha na kufasiri, na kurukaruka juu-na-chini na kucheza katika roho; kunywa damu kwa kutumia fuvu la kichwa cha binadamu, na kulaani Jina la Yesu Kristo.

69 Unasema, "Mimi ni wa kanisa. Haleluya! Utukufu kwa Mungu! Mimi … " Wewe ni wa nini? Kanisa ni Neno! Na Neno linasema, "Ni aibu kwenu kufanya hilo."

Enyi kundi la Mafarisayo mliopofushwa macho mkiwaongoza wale watoto wadogo wasikini kwenda jehanamu namna hiyo; kwa sababu mnaogopa tikiti ya chakula na mtafukuzwa kwenye dhehebu lenu kama mkianza jambo kuhusu Hilo. Muone aibu, ninyi wanafiki! Oneni aibu kwa hilo. Mkiona saa ikikaribia namna hii, na unageuzwa na mila zako kutoka kwenye Neno la Mungu. Mtathubutuje ninyi mliopofushwa macho!

Je, Biblia haisemi kuwa ninyi mmepofushwa macho? Huwezi kuelewa kuwa u kipofu? Biblia ilisema ulikuwa kipofu. "Na uko uchi, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu, nawe hujui." Unapofikiri una kanisa kubwa kuliko yote mjini, na unafanya hili, lile, au lile lingine; na Biblia ilisema u masikini uwezavyo kuwa, na u kipofu. Na Yeye bado amesimama mlangoni akijaribu kukuuzia dawa ya macho; sio kukuuzia, bali kukupa, nawe huipokei. Unayatimiza Maandiko.

70 Ni siku gani mnyoishi watu? Mnatambua ile saa, mnatambua ile ishara?

Wangeweza tu kutambua, wale wanawake, kuwa huyo ni Ibilisi. Ni pepo la utovu wa heshima, katika jina la dini. Amekuwa hivyo siku zote. Alikuja kwa kila nabii, alikuja kwa kila mwenye hekima, alikuja hata kwa Yesu Kristo, kama mtu wa kidini. Na Biblia ilisema "angekuwa karibu mno katika siku za mwisho," hata Wapentekoste. "na angewadanganya wale wateule halisi," kutoka katika kanisa la Pentekoste, "kama ingaliwezekana." [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.]

"Wachache," Yeye alisema, "kwa sababu mlango ni mwembamba na njia imesonga, na lakini ni wachache watakaoiona. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo nafsi saba ziliokolewa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Liwazie! Tunaishi katika siku gani? Unatambua saa hii, unatambua siku hii? Nachukua mno wakati wenu, lakini nina dakika chache zaidi. Unaona?

71 Kuwafanya wakate nywele zao. Vema, wanasema, "Kanisa letu halijali hilo." Unajua ni kwa nini? Wao ni vipofu. "Si tatizo kukata nywele zenu." Biblia inasema ni tatizo! Hata ni jambo la utovu wa heshima kwa wewe hata kukata nywele zako, na hata kuomba. Unasema, "Vema, mwanamke inampasa afunikwe." Na Biblia ilisema kuwa "nywele" zake ni kifuniko chake. Sio kofia; nywele zake.

Vipi kama Musa angalisema, "Nitavua kofia yangu badala ya viatu vyangu."? Lisingefanya kazi. Mungu alisema "viatu," na Mungu alimaanisha viatu. Alisema "nywele," sio kofia! Utukufu kwa Mungu! Yeye alipenda hilo, nina hakika. Mungu asifiwe! Yeye humaanisha kile tu Yeye anachosema. Maandiko hayafasiriwi kama mtu fulani apendavyo. Hayamaanishi kwa dhehebu lako tu; Yanamaanisha kile yanachosema, na Yeye Ndiye mfasiri.

72 Unasema, "Namjua mwanamke anayefanya hivyo." Sijali kile unachojua. Najua kile Mungu alichosema kuhusu hilo. Unajiridhisha mwenyewe.

Kama tu wangeweza kutambua hicho ni kitu gani, bibi. Uh! Kama tu ungeweza tu kutambua! Au, "mwanamke," sio bibi.

Niliona ishara, ikishuka chini kutoka kwenye Nguruwe dume wa rangi ya bluu, kuelekea chini, naamini ni pale Fifth Street, ukumbi wa pombe, ikasema, "Meza kwa ajili ya mabibi." Nilisimama tu pale; nikasema, "Kamwe hujawahi kunywa hata moja." Bibi mwadilifu hawezi kwenda mahali kama hapa. Mwanamke anaweza, lakini sio bibi mwadilifu.

Uliona, kuanguka kwa ulimwengu, kulianza na uovu wa mwanamke? Unajua utaishia kwa njia hiyo hiyo, uovu wa mwanamke? Na kanisa huwakilisha, ni kwa mwanamke, kanisa ni mwanamke, nikinena kiroho. Vivyo hivyo na Bibi arusi ni mwanamke, nikinena kiroho.

Uovu wa kanisa, jinsi unavyofanyka! Tazama maono, tazama yale mambo, angalia hata yale maono anayotoa Mungu, na lile ono ni kweli. Ninayo Biblia yangu juu ya moyo wangu, kwenu ninyi watu kwenye kanda, na kusanyiko linaweza kuona. Nililiona hilo! Mungu Mwenyenzi anajua hilo ni Kweli. Sikuwahi kujua hadi sasa hivi. Yuko pale, "uchi, naye hajui." Alikuwa tu na wakati mkuu. Ndilo hilo. Lakini yule Bibi arusi mdogo alipotokea, ilikuwa tofauti. "Alfa na Omega." Uh-huh.

73 Ibilisi hufanya hilo. Lakini kama wale Wayahudi wa zamani, wanapoliona Neno … Na Yesu alisema kwa akina, Yeye aliwaambia hili wanafunzi Wake, "Mnayachunguza Maandiko. Mna-mnajikanganya kuhusu Mimi na huduma Yangu. Mnayachunguza Maandiko. Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, nayo yananishuhudia Mimi, yanawaambia Ujumbe Wangu ni nini. Ikiwa hamwezi kuniamini Mimi, aminini Maneno yale yale ambayo Mungu anawafasiria kwenu."

"Hatuwezi kuwa na huyu Mtu atutawale. Tunao makuhani wetu wenyewe, na kadhalika." Endeleeni basi, hilo ndilo linaloweza kusemwa. Mmechelewa mno, hata hivyo. Desturi za kidhehebu zinazosema ni sawa, wanazisikiliza hizo. Ni heri wangesikia … Mnaamini ne-neno la-la mwanadamu kuliko unavyoamini Neno la Mungu.

Hawatambui. Makanisa leo hii hayatambui Timotheo wa Pili 3. Ikiwa …

74 Nawaona baadhi yenu mkiandika Maandiko. Sasa, haya ni Maandiko ninayonukuu kutoka hapa hapa. Ambapo, ikiwa mtu yeyote akiniuliza juu yake, au mkono wangu juu yake, naweza kuwaonyesha Andiko kwa ajili yake. Unaona?

Hawatambui Timotheo wa Pili 3, pale yaliposemwa, "Katika siku za mwisho watu watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wanaowadharau wale walio wema (Bibi arusi) unaona; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. Kwani hii ndiyo aina ya watu itakayokwenda nyumba hadi nyumba, na kuwaongoza wanawake wapumbavu, wanawake wapumbavu huongozwa na tamaa, kamwe hawajifunzi au kamwe hawawezi kuja kwenye maarifa ya ile Kweli." Kamwe! Wasingefanya hilo, na hawalifanyi. Mungu alisema hivyo. "Na, Farisayo kipofu, huwezi kuliona? Sijakasirika; ninapigilia tu msumari ndani na kuukaza. Wala kanisa halilitambui Hili. Wanawake hawawezi kulielewa. Wanapaswa … "Wanawake wapumbavu, huongozwa na tamaa," Hollywood, namna zote hizi za vitu, nywele zilizokatwa, wakivaa kaptula, wakijipodoa, namna zote hizi za vitu, ambavyo havifai.

Je, unajua wanawake wamehitimisha sehemu kubwa katika siku za mwisho?

75 Unajua Biblia ilisema, kwamba, "Wale watakaoepuka hii laana kuu watakuwa tawi jema mbele za Bwana"? Siku fulani nitalifikia, Bwana akipenda, kwa ajili yake, kwa ajili yenu wanawake. Mpate kuona kile Mungu anachowazia wanawake ambacho huepuka hasa laana ya siku hii. Akasema, "Yeye atakuwa mzuri."

Nilimsikia mwanamke, siku ile, akicheka … Msichana, kundi la wanawake walio nusu uchi, wenye uadilifu wa hali ya chini kuliko-kuliko mbwa jike, wakimcheka mwanamke mzee mwenye nguo ndefu. Sikilizeni hapa, enyi wanawake mliopindishwa kidogo, yeye anacho kitu fulani ambacho hamkijui. Anao uadilifu. Hata hamjui jina hilo ni nini. Mlilipotezea kwenye kitanda cha utotoni. Hata hamjui jema na baya; yeye anajua. Yeye anacho kitu fulani kilichofichwa ndani ya moyo wake ambacho hamkijui. Ninyi mlikipoteza; kamwe hamtakipa. Msimwite wa mtindo wa kale, na kadhalika, namna hiyo. Yeye anajua jambo fulani ambalo hamlijui. Yeye ameficha ndani ya moyo wake, hazina ya uadilifu. Ninyi hamjui hata

neno moja kuhusu hilo. Mama yako alikulea hivyo. Mchungaji wako aliliruhusu; inaonyesha pale alikosimama. Nahubiri kumhusu yeye hapa hapa sasa. Unaona? Mnaona pale mlipo, ninyi makanisa?

76 Yesu alisema, "Maandiko haya yote lazima yatimie" Na yametimia.

Tazama, "Kama Yane na Yambre walivyompinga Musa," atakuja moja kwa moja, baadhi yao. Siyo sasa, hazungumzii Methodisti, Baptisti hapa, hawako hapa. Unaona? "Lakini kama Yane na Yambre walivyompinga Musa na Haruni, vivyo hivyo na wao; mtu aliyeharibikiwa akili kuhusu ile Kweli." Wakiwa wamepotoka na kuingia katika kanuni na mafundisho ya kanisa badala ya Biblia. Na ndipo Yane na Yambre wangeweza kufanya chochote ambacho Musa angefanya. Unaona, "kama Yambre," unaona ulinganisho pale? "Kama Yane na Yambre walivyompinga Musa, vivyo hivyo hawa watu walioharibikiwa akili zao kuhusu ile Kweli, wakilikataa," hawawezi kuwa Nalo katika ujirani yao, hata hawawezi kushirikiana Nalo, hawatakuwa na uhusiano Nalo. Lakini alisema, "Upumbavu wao utadhihirika." Yule Bibi Arusi atakapokaa mahali pake na kwenda angani, itajulikana, usijali; kama Musa, alipowachukua wana wa Israeli, na wakakimbia kutoka Misri, na Misri ikazama. Vema.

77 Yesu alisema, "Maandiko yote yametolewa kwa uvuvio, kwa hiyo Maandiko yote lazima yatimie." Wakati yeye … Walimwuliza Yeye wakasema, "Unajifanya Mwenyewe kuwa Mungu."

Akasema, "Ninyi, katika sheria yenu wenyewe huwaita wale manabii ambao Neno la Bwana liliwajia, mliwaita 'miungu,' na ndivyo walivyo." Akasema, "Basi ni jinsi gani mnaweza kunihukumu Mimi nisemapo Mimi ni Mwana wa Mungu?" Haya Maandiko yote yanatolewa kwa uvuvio; yote lazima yadhihirishe, yote lazima yatimizwe. Angalia kule, walikuwa vipofu mno, walikuwa wametekwa mno na neno la mwanadamu, badala ya kutekwa na Neno la Mungu. Hilo ndilo huwafanya wanawake watende hayo. Hilo ndilo huwafanya wahubiri watende hilo. Wametekwa na askofu badala ya Yesu. Wametekwa ndani yake, na-na mfuko wao wa fedha, kusanyiko kubwa.

78 Angalia tu kama mimi ninapendwa na watu. Chukuwa watu wanaotoka nje ya Jeffersonville, pamoja na kundi dogo linalotokea hapa Jeffersonville; chukua hawa wa nje, ya Jeffersonville, uwatoe hapa hekaluni asubuhi hii, nisingekuwa au sina watu nusu dazeni ya kuwahubiria. Ni kitu gani? Kanisa hili limeundwa na nchi nzima; kutoka New York, kutoka Masschusetts, hadi Boston, Maine, hadi baharini, Georgia, Alabama, na kote nchini. Wanakusanyika pamoja. Amina! Hilo ndilo Yeye alilosema. "Kutakuwa na Nuru wakati wa jioni."

Wao hawawezi kutambua Nuru ya jioni. Hilo ndilo tatizo. Yeye halitambui tu Hilo. Ni kipofu kupindukia. Biblia ilisema yeye angekuwa hivyo.

79 Russia imepata mahali pake ulimwenguni, katika sayansi, si zaidi ya kwenye miaka arobaini iliyopita, Unajua, wakati Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia vilipotokea, hawakuweza kamwe … waliidharau Russia. Ndugu Roy … Lilikuwa tu kundi la wajinga Wasiberia wakubwa wa zamani, sharafa kote kwenye nyuso zao, na hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto. Hiyo ni sahihi, Russia, lakini ilitambua nafasi yake. Ilipasa ifanye hilo ili kutimiza Maandiko. Mnajua utabiri wangu wa kile nilichosema kingetokea, jinsi wote wangekusanyika katika ukomunisti. Sasa inaongoza ulimwengu katika sayansi. Tuko mbali nyuma yake. Ulimwengu wote uliobaki uko nyuma yake. Inaongoza nafasi yake. Imetambua tu kuwa walikuwa na watu wenye akili pia.

Angalia, binadamu anazo zile zile hisi sita alizokuwa nazo miaka elfu sita iliyopita. Miaka elfu sita iliyopita, kwa hisi sita alizokuwa nazo, aliwasiliana na makao yake ya kidunia na kumtumikia Mungu. Na sasa, katika miaka sabini na tano iliyopita, yule mwanadamu ametoka kwenye gari linalokokotwa na farasi hadi kuwa mwana anga. Kwa nini? Aligeuka kutoka kwenye imani yake kwa Mungu, na kuigeuzia kwenye hisi zake na uwezo wake kama mwanadamu. Uliliona hilo? Aliacha kumtumainia Mungu. Anajitumainia mwenyewe.

80 Kama huyu mwanamke kafiri. Jina lake ni nani, Washington pale, lililogeuza lote hili? [Mtu fulani anasema, "Murray."-Mh.] Jina lake nani? ["Murray."] Murray alisema, "Ili mradi tuna jeshi la nchi kavu na la wanamaji, hatumhitaji Yehova wa zamani." Lo-lo- sijali tuna nini. Kwangu mimi ni Yehova au hatuna chochote. Hebu jeshi la nchi kavu na jeshi la wanamaji lizame, na litazama, lakini Yehova atakuwepo milele. Na ili mradi mimi ni sehemu Yake na Mwana Wake, nitabaki Naye daima; sio kwa wito wangu au chaguo langu, ila kwa uchaguzi Wake. Amina, amina! Sihusiki na hilo. Ni Yeye anayehusika! Unipe Yeye au unipe kifo. Mataifa yainuke na kuanguka; Yehova atadumu. Yeye amefanya hilo, kote katika vipindi, Rumi ilipoanguka, Misri ilipoanguka, na wale wengine wote walianguka. Na Yeye bado anadumu Yehova. Lo, haleluya! Najisikia kubarikiwa.

Sababu ya Russia kujitambua, ilipasa ifanye hivyo. Kama tu Israeli ilivyopasa kurudi katika nchi ya nyumbani. Ilimpasa Mungu amrudishe Israeli nchini mwake, kwa ajili ya Baragumu. Na vivyo hivyo Mungu aliisukuma Russia kwenda juu kule, katika ukomunisti, ili ifanye kile hasa kilichotabiriwa kuwa ingefanya.

81 Mwanadamu na hisi zake sita amekuwa katika nyakati zote kwenye gari la kukokotwa na farasi,

akimtumainia Mungu. Katika miaka sabini na tano iliyopita, aliacha kumtumaini Mungu. Walipotia saini katiba ya hii Marekani, walimweka Mungu katika kila walichofanya. Sasa hawana hata mkutano, na kamwe hata hawataji Jina Lake. Hiyo ni sahihi. Wanategemea ubora wa sayansi yao kuvutia kwa, wao, ubora wa sayansi yao kuvutia kwa sayansi yao, au kikundi maalum kinachobuni uharibifu. Hiyo ni sahihi hasa. Ulimwengu wote umemezwa katika kutokuwa na maarifa ya Biblia-Biblia. Ulimwengu wote umemwacha Mungu. Lakini, waza tu, pale pale katikati ya hilo lote, na makanisa ya kidhehebu na uharibifu wote wa seminari zao na kila kitu, Mungu ametumia Neno la nabii Wake na kumchonga Bibi arusi atakayeamini. Alisema Yeye angefanya hilo. Yeye amemkata kutoka kwenye hilo jambo kile Yeye alichoahidi angefanya.

Wanategemea werevu wa kibinadamu, sayansi yao ya kiinadamu, na kadhalika; walimwacha Mungu nje, Ambaye alimtumainia hapo awali. Marekani imemwacha Mungu nje. Hata walimtoa Mungu nje ya shule, kwani watoto wetu wadogo hawawezi hata kusikia kumhusu Yeye. Walimtoa nje ya shule. Sasa wanajaribu kumtoa kwenye dola, "Tunamtumaini Mungu." Wanakwenda kuindoa ahadi ya utii kwa bendera, "Taifa moja chini ya Mungu." Wanakwenda kuondoa hilo.

82 Tazama wamekwenda kwenye hisia zao wenyewe na hisi zao wenyewe. Kwa sababu, katika miaka sabini na tano iliyopita, yeye hajabadilika hata kidogo katika hisi zake, bado yeye ni mtu yule yule aliyeumbwa na Mungu hapo mwanzo. Lakini, katika hizi siku za mwisho, huwezi kutambua pale tuliko? Na kanisa limemwacha Mungu, kwenye hilo, likageukia kwenye ujuzi wa seminari, na kadhalika, badala ya Neno. Hata hawamtambui Yeye katika mikutano yao, katika mashule yao, au chochote, zaidi.

Israeli, katika miaka sabini na tano iliyopita, ametambua kitu fulani kimewaleta nchini mwao, kama ilivyoahidiwa. Hawajui lilivyofanyika. Waliteseka kama nini, kuuawa kikatili, chini ya zile Baragumu, lakini wako nchini mwao. Hawajui ni kwa nini.

83 Kwa nini Russia iliamka? Kwa nini mataifa yaliamka? Kwa nini mwandamu ameweza kufanikiwa? Walati wanasayansi, miaka mia tatu iliyopita, mwanasayansi wa Kifaransa aliviringisha mpira kwenye mwendo kasi fulani kukatisha dunia, na kuthibitisha, kwa utafiti wa kisayansi, "ikiwa binadamu angefanya mwendo kasi mkubwa wa maili thelathini kwa saa, mvutano ungemwondoa huyo mtu kutoka juu ya uso wa nchi; kulingana na uzito wake, kulingana na uzito wa mpira." Sasa anakwenda maili elfu kumi na saba kwa saa, unaona, bado akijaribu kupanda. Alitambua hilo hivi karibuni tu. Kwa nini? Inabidi awe hivyo.

Mbona, kanisa lilikuwa linasimama juu ya mwamba wa Yesu Kristo. Haidhuru kitu gani mtu yeyote alisema, wao walidumu na lile Neno, ule ujumbe wa saa hiyo; Luther, Wesley, na moja kwa moja hadi kule. Na sasa wamerudi kwenye mapokeo. Kwa nini limefanya hilo?

Miaka ishirini na tano iliyopita, Israeli imetambua tu kuwa wako kwenye nchi yao kwa ajili ya jambo fulani. Lilitabiriwa wangekusanyika tena; Hosea alisema hivyo. Tulilisoma kitambo kilichopita. Mungu tusaidie kulielewa hilo! Vema.

84 Wakati huo huo, yule Bibi Arusi ametambua ile Nuru ya jioni, ameanza tu kutambua. Wapentekoste wenye njaa wameanza kutambua kuwa yale mashirika hayana chochote walichokuwa wanakitafuta, wamepotoka mno na kugawanyika. Unaona, ni wakati wa utambuzi, utambuzi. Inakupasa utambue. Ulimwengu umekwishatambua. Mataifa yamekwishatambua. Sayansi imekwishatambua. Ibilisi amekwishatambua ni wakati ambao yeye anaweza kuwaharibu wanawake, kuharibu kanisa, kuharibu watu. Yeye ametambua hilo. Na Mungu ametambua kuwa kuna watu duniani ambao Yeye aliwachagua tangu asili kwa ajili ya Uzima. Yeye alitambua hilo katika wakati wa kutuma Ujumbe Wake. Yeye amekwishalifanya hilo. Watu wamekwishatambua Hilo, wakati wa Bibi arusi amekwishatambua ile Nuru ya jioni.

Laiti Sodoma ingetambua siku zake, ilipoona wale wajumbe wakija kule, kama Billy Graham na Oral Roberts!

85 Sasa, mtu fulani asiye mwadilifu kule Phoenix alisimama tu na kusema … alicheza ile sehemu kwenye-kanda, na kusema mimi nilisema hapa, "lazima nibatizwe katika Jina la Yesu." Kasema hivyo, na halafu akasema, "Sasa unaona hapa, alisema hapa …" Nilipokuwa nikizungumza kuhusu Afrika, jinsi walivyobatiza mara tatu mtu akiwa ametazama mbele na akiwa amegeukia nyuma. Akasema, nilisema, "Haina tofauti yoyote." Unaona, kamwe hakuicheza sehemu iliyosalia ya kanda; ile sehemu tu, na kuizima. Ambapo, ingekuwa kosa la kujutia kufanya hilo. Zile kanda ziko chini ya umiliki wangu kabisa kisheria. Hakuna mtu wa kuzichafua. Nivyema usifanye hivyo. U-u-una sheria itakukabili. Lakini tungefanya hilo? Hapana. Akasema, "Waache wenyewe." Mungu aliniambia kile kitakachotokea. Tazama tu, weka tu jicho lako kwa yule mtu. Unaona?

86 Wakati uo huo Bibi arusi ameipata ile Nuru ya jioni. Laiti Sodoma wangetambua saa yao!

Sasa, mtu huyu huyu aliweka kanda, akasema, "Tazama hapa, kwenu ninyi Wapentekoste," akasema, "na ninyi Wabaptisti. Huyu mtu, nabii wa uongo, William Branham," unaona, "amesema kuwa Oral Roberts

na Billy Graham walikuwa Sodoma." Unaona, halafu akasimamisha ile kanda; hayo tu, unaona. Hakuendelea mbele iliposema, kuwa, "Wao walikuwa wajumbe kwa Sodoma." Sio kuwa ndani ya Sodoma. "Walikuwa pale kama mjumbe aliyetumwa Sodoma." Mtu yeyote anajua nilisema hilo. Cheza kanda yako. "Yeyote atakayeondoa au kuongeza, huyo ataondolewa mbali kutoka kwake." Ni Neno la Bwana. Linasimama hivyo.

87 "Kama Sodoma ingemtambua mjumbe wake, ingesimama hadi leo," Yesu alisema, ikiwa ingemtambua vile vile kama Abrahamu alivyomtambua. Abrahamu alijua kulikuwa na mwana aliyeahidiwa aliyekuwa anakuja. Lakini alijua kungekuwa na badiliko la namna fulani, kwa sababu alikuwa mzee kupindukia, na Sara vivyo hivyo. Lakini alipomwona yule Mmoja Abaye angeweza kutambua yale mawazo ya Sara, nyuma Yake, Yeye alitambua ile saa aliyokuwa anaishi. Akasema, "Bwana wangu, ngoja nichote maji kidogo hapa na kukuosha miguu Yako." Walikula kipande cha mkate. "Hebu nikuombe Wewe, kawia tu kidogo," unaona, hapa, "B-w-a-n-a wangu," herufi kubwa B-w-a-n-a, "Elohim." Yeye alitambua kuwa Mungu alikuwa anazungumza naye akiwa kwenye mwili wa mwanadamu. Alitambua ishara yake, na alibarikiwa na Bwana. Sodoma hawakutambua siku yao, na iliteketezwa. Yesu alisema, Kama ilivyokuwa katika siku ile, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Mungu ata- … au Mwana wa Adamu atakapodhihirishwa."

88 Sasa, kanisa halijatambua siku yake. Kama Israeli, ilivyolazimishwa kurudi Palestina, kanisa litalazimishwa kuingia Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Kwa nini? Halikutambua saa yake. "Enyi watu, tokeni kati yake, msishiriki dhambi zake!" Kimbiza, uzima wako, au utapatwa na alama ya mnyama na huwezi kufanya chochote kingine kuhusu hilo. "Aliye mchafu na azidi kuwa mchafu. Aliye mtakatifu, "sio atakuwa mtakatifu, "mtakatifu sasa. Aliye mtakatifu," sio aliyepunguza, mwanamke aliyefupisha nywele; hawezi kuwa. Sasa, hilo linaonekana wazi mno, lakini hilo ni Andiko. Biblia inasema, "Anaaibisha kichwa chake," na kichwa chake ni mume wake. Kichwa cha mume ni Kristo. Hivyo mwanamke anamwaibisha Kristo. Atawezaje "Kuwa mwenye kuaibisha" bila kuwa "mchafu"? "Yeye aliyefupisha nywele awe hivyo hivyo. Mwanamke avaaye kaptula aendelee kuivaa. Yule alikanaye Neno aendelee kulikana Hilo." "Lakini yeye aliye mtakatifu aendelee kuwa mtakatifu. Yeye aliye mwenye haki aendelee kuwa mwenye haki; Neno la haki la Mungu, Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa. Endelea kuwa mtakatifu, endelea kuwa mwenye haki!" Tambua! Ndiyo, bwana.

Siku.... Sio kanisa halijatambua siku yake,

89 Kama Israeli, akirudi chini ya ahadi, hajui alivyorudi pale. Aliwekwa tu pale kwa nguvu isiyo yake mwenyewe. Kwa nini? Nguvu ya taifa ilimweka mahali pake. Sasa nakwenda kusema jambo fulani. Nguvu ya taifa ilimweka Israeli katika nchi yake ya nyumbani; nguvu ya taifa italiweka kanisa katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni; lakini nguvu za Mungu zitaweka watu katika Bibi arusi. Ulimwengu husukuma huku na ulimwengu husukuma kule, lakini Mungu husukuma kuelekea juu. Roho wa Mungu, ambaye ni Neno la Mungu, "Neno Langu ni Roho na Uzima," atamweka yule Bibi arusi mahali pake. Kwa sababu yeye atatambua nafasi yake katika Neno, basi yuko ndani ya Kristo, atamweka Bibi arusi mahali pake. Hakuna nguvu ya taifa italifanya hilo. Lakini nguvu ya taifa iliipeleka Israeli nchini mwake; nguvu za taifa za Baraza la Makanisa zitapeleka kila shirika kwenye hilo; lakini Nguvu za Mungu zitamwinua Bibi arusi hadi kwenye Utukufu, kutoka kwenye hilo.

Ee, watu, tambueni siku yenu, kama Yesu alivyowaonya; ile ishara ya Sodoma, na hali ya kanisa ya siku hii.

90 Tazama kile Yeye alichosema kingetokea katika hii siku. Kisikilize kwa makini. Ile ishara ya Sodoma ingetokea katika hii; ishara kama ya Abrahamu, ile siku kabla ya Sodoma, ile walioitwa nje. Mambo haya yote yaliyotabiriwa, yatakuwa yanatokea sasa. Tazama ile siku unayoishi. Tumepita juu ya na kupita juu yake.

Sasa Yeye ameahidi kuwatumia Nuru ya Mbinguni, kuivisha ile Mbegu ya Neno ile itakayopandwa kwa ajili ya hii siku. Ile Mbegu iko ndani Hapa. Ile Mbegu iko katika Biblia. Kwa nini? Yesu alisema hivyo. "Neno ni Mbegu aliyopanda mpanzi." Na sasa, kabla hujawa na zao lolote, haidhuru kama umepanda mbegu, inapasa ipate nuru kuipevusha ile mbegu, la sivyo itaoza na haitakuwa na maana; itapotea. Lakini kama ina mbegu ardhini, ardhi inayofaa, yenye mwanga sahihi wa jua juu yake, inapasa ipevuke. Na Yeye aliahidi kuwa katika siku za mwisho, katika wakati wa jioni, Mwana angetoka kuipevusha ile Mbegu. Ile Mbegu inahubiriwa. Mwana wa Mungu anaipevusha ile Mbegu, kwa kuidhihirisha, kuifanya itoke nje mbele yako na kuthibitisha kuwa Hiyo ni sahihi. Je, unalielewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Tambua siku yako.

Ninafunga sasa. Ni wakati wa kufunga sasa.

91 Na Laodikia iliyo tajiri, iliyopofushwa, yenye elimu italiondoa Neno litoke kati yao. Wamelifanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Yeye alisema wangefanya hivyo. Kama wale manabii wa kale walivyotumwa kuthibitisha Neno lililoahidiwa la siku yao, ili kwamba watu waliochaguliwa tangu asili, siku yao, waliliona. Kama yule mwanamke pale kisimani, kama Nathan, kama kipofu Batimayo, kama Petro, na wale wengine waliolitambua. Yeye alikuwa lile Neno. Na matendo, "Kama sitendi kazi zile Baba alizoahidi

ningefanya, basi msiniamini Mimi. Lakini kama nafanya zile kazi, ingawa hamniamini Mimi, amininі zile kazi. Zinawashuhudia Mimi ni nani.” Unalielewa? Vema, usiikose ile siku, iliyotumwa. Wanaume na wanawake wa siku nyingine walilitambua, na wakaingia ndani na wakawa salama.

Wapentekoste, ee, jamani, kwa nini hamtambui siku yenu? Tambueni ile siku ya wakati wa jioni. Iko hapa, na iko hapa, kwamba, ithibitishe kule kuja kwa Kristo, kuithibitisha. Tuko mwishoni. Tambua siku yako.

92 Najua nimewaweka muda mrefu. Ni saa sita sasa. Lakini, napenda hiki Chakula, Huu ni Uzima. Ni Uzima. Ni Uzima, kwa mwamini. Tambueni ile siku mnayoishi, na ishara ya wakati.

Ona pale kila kitu kilipo; Israeli.; lilipo kanisa; uovu ulipo; Bibi arusi alikosimama. Kumebaki nini? Jambo linalofuata, kumchukua Bibi arusi juu. Bila shaka, kila kanisa linatazamia jambo kuu. Pentekoste husema, “Utukufu kwa Mungu!Itakuja siku watakapofanya hili, na wanakwenda kufanya lile. Unaona, wao ni maprofesa. Wanaamini.

Kama, wakati mmoja, Kayafa alisema, “Je, si ni sahihi mtu mmoja afe, na siyo taifa lote liangamie?” Biblia ilsema yeye alikuwa kuhani mkuu, ndiyo sababu akasema hilo. Yeye alitabiri, bila kujua kile alichokuwa anasema. Lakini alitambua ukweli wake halisi, kwamba alikuwa anamtoa dhabihu Mungu hasa ambaye alidai kuwa kuhani mkuu wake? Ndivyo hivyo leo! Wanatazamia pale mahali fulani, kuja kwa wakati mkuu.

93 Mbona huwa nakwenda nao katika mkutano wa Wafanya Biashara. Wanasema, “Utukufu kwa Mungu!” Wale wahubiri husimama na kulisisimua kusanyiko, na kusema, “Unakuja uamsho mkuu. Mkono wa Bwana utakuwa juu ya nchi!” Na jinsi iliyoje watu wanakwenda mbele, wakikimbia kama … Na hawatambui hili liko chini ya Baragumu za Israeli. Kwa nini wanafanya hilo? Ni kwa sababu wao ni maprofesa wa Kikristo, na hawatambui. Wala Kayafa hakutambua kile alichokuwa anafanya. Na wao hawatambui kuwa wameukataa Ujumbe hasa uliotumwa kwao. Amina!

Kila sehemu ya Maandiko, tumepitia siku baada ya siku, na juma baada ya juma, hadi ni Kweli isiyowezekana kupingwa. Yesu alisema, “Ikiwa kipofu hawezi kuipokea,” waache. Kama kipofu akimwongoza kipofu, wote watatumbukia shimoni.“ Sijui ni lini, sijui ni wapi, lakini najua inakuja.

94 Mnajua, naona ni kwa nini Shetani hakutaka nifanye hili. Jana, nilijisikia vibaya mno. Sikuweza kupata Neno kutoka kwa Bwana. Nilifanya kila kitu nilichojua kufanya, na sikuweza. Na asubuhi hii, nilipoamka … nikala mahindi, jana, na ikawa kama yamelala pale pale tumboni mwangu. Niliugua mno, siku-sikuweza tu kulipata. Nikawaza, “Ulimwengu una tatizo gani? Nakwenda kule chini, na sijui nakwenda kusema nini. Na, Bwana, siwezi hata kupata Andiko mawazoni mwangu, la kuandika. Sipati kitu.” Sikujua tu la kufanya. Ndipo, baada ya Ujumbe kuanza kunijia, Shetani akaendelea kusema, “Unajisikia vibaya kupindukia. Kichwa chako kinauma. Unaumwa. Huwezi kwenda chini kule. Huwezi kusimama pale. Itakuwa hivi, itakuwa vile.”

95 Nakumbuka, wakati mmoja, hadithi ya mtu mmoja mdogo mzaliwa wa London kule Uingereza. Yeye alikuwa mtu wa kawaida tu. Na walisema kuwa m-m-mfalme, mmojawapo wa wafalme katika siku za mwanzo alikuwa anakwenda kwenye jumba lake la mfalme. Na huyu, yeye hakuwa na yeyote … Yeye alikuwa na ujumbe wa kupeleka, ujumbe wa haraka, kwa sababu ya adui. Na hivyo, aka-aka-akamwambia huyu kijana mdogo aliyesimama pale, akasema, “Hapa, chukua huu ujumbe, chukua huu ujumbe! Harakisha kwenda mahali fulani-fulani, na uamrishe hili lifanyike.” Na kasema, “Chukua fimbo yangu mkononi mwako. Hiyo itakuthibitisha, kuwa mimi … umetumwa kutoka kwangu.”

Naye akaichomeka chini ya vazi lake, na akaondoka. Walinzi wakimsimamisha kila mahali, kila mtu mwingine. Akipiga kelele, “Ondokeni! Nina ujumbe wa mfalme.” Amina. “Mimi ni mjumbe wa mfalme,” neno lililothibitishwa.

Nikawaza, “Shetani, ondoka njiani mwangu! Nina Ujumbe wa Mfalme. Lazima niende! [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara kadha-Mh.]

96 Wakati mmoja walipomuua Mfalme wa Amani, na kumweka kaburini, na kufunika kaburi, na kifo kikamshikilia kwa siku tatu mchana na usiku. Lakini mnamo Pasaka asubuhi Yeye alikuwa na fimbo ya mfalme mkononi Mwake, na kupiga kelele, “Ondoka kifo! Ondoka kaburi! Funguka! Mimi ni Ujumbe wa Mfalme. Lazima nije kuthibitisha huu ufufuo. Mimi ni ufufuo na Uzima.” Haleluya! Najisikia vizuri kweli kweli sasa. Ni Ujumbe wa Mfalme. Hebu tutambue marafiki, kwani tumeitwa kukusanyika pamoja kwa ajili ya kupigwa kwa Baragumu.“ Kwani Parapanda ya Bwana italia, ndipo hakutakuwa na wakati tena.”

Yeye amewakusanya Israeli. Zile siku tatu, katika siku ya tatu Yeye alisema angefanya hilo. Miaka elfu mbili na mia saba imekwishapita. Katika ile siku ya tatu Yeye alisema angewakusanya pamoja, na Yeye amekwishafanya hilo. Yeye alisema amekwishafanya njia ya Uzima. Ndivyo hivyo, kusubiri tu sasa kuondoka kwa Bibi arusi njiani ili wao waje, wale manabii wawili, manabii Waebrania watakaotambua.

97 Mnakumbuka mimi nikiwa nimesimama Cairo, kwenda juu kule, wakati Lewi Pethrus aliposema, "Ndugu Branham, ikiwa wangewahi kuona na hilo … Wao wanaamini manabii wao."

Nikasema, "Ni jambo jema kwangu." Unaona jinsi mwanadamu alivyo? Lakini unaona neema ya Mungu? Nikasema, "Nitalisoma hili Agano Jipya." Walilisoma kule, Ndugu Lewi aliwapelekea, zaidi ya milioni, kule, Ndugu Lewi Pethrus kutoka Sweden. Walisoma Hilo, wakija juu na chini kule, wale Wayahudi; sio kama hili kundi la Wayahudi wa kisasa, bali katika nchi yao ya nyumbani. Na kaja chini, akasema, "Ikiwa huyu ni Masihi, hebu tumwone akitenda ishara ya nabii, tutaamini hilo."

Lewi Pethrus akasema, "Ndugu Branham, hiyo hapo nafasi. Hiyo hapo nafasi." Mtu mmoja aliniambia kuwa, hiyo ingekuwa nafasi. Nikaenda," akasema, moja kwa moja kwenye hilo."

Mtu fulani akaja na kuketi pale, Ndugu Arganbright, akasema, "Ndugu Branham, hilo litawatahadharisha tu Israeli! Liwalete nje mbele ya Hilo, na kuwaonyesha ishara ya nabii. Wataliamini Hili."

Nikasema, "Bwana, niko hapa tayari." Nikarukia kwenye ndege; nikachukua fedha na kupata tiketi; nikatua Cairo. Nikasema, "Naam, niko tayari."

Roho Mtakatifu akasema, "Hapa sio mahali pako. Huu sio wakati wako." Unaona, umejitanguliza mbele mwenyewe. Nikawaza, "Loo, jamani! Nimekuja kote hadi hapa; ni-nitakwenda."

Kitu fulani kikasema, "Simama hapa hapa! Usiende kule. Geuka kuelekea India. Usiende kule. Nenda India, lakini usiende kule."

98 Nikawaza, "Kwa nini?" Nilipokuwa nikitoka nyuma ya sehemu kunakoning'inizwa ndege, nikasema, "Bwana Yesu, hili lina maana gani?" Ndipo Yeye akanifahamisha. "Hakuna Mataifa. Hawa manabii ndio wenyewe." Inapasa iwe kulingana na Maandiko. "Musa na Eliya inapasa waje." Na, zaidi, Bibi Arusi hajaondolewa njiani bado. "Na wale manabii watarudi na watafanya ishara ya nabii." Hayo ni Maandiko. Yote yatakuwa yametimia pale basi, kikamilifu, Israeli kama taifa litazaliwa katika siku moja. Amina! Nuru za jioni zinang'aa!

> Kutakuwepo Nuru wakati wa jioni,
> Hakika utapata njia ya Utukufu;
> Katika njia ya maji pana Nuru leo,
> Kuzikwa katika Jina la Yesu la thamani;
> Tubuni dhambi zenu, vijana na wazee,
> Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;
> Nuru za jinoni zimekuja,
> Ni ukweli kuwa Mungu na Kristo ni Mmoja.

99 Tuko penye wakati wa mwisho rafiki. Na ndipo tunawazia huu wimbo wa mwandishi aliyevuviwa, aliposema:

> Mataifa yanavunjika, (hii ni kwenye
> miaka kumi na tano iliyopita),
> Israeli inaamka
> Zile ishara walizotabiri manabii;
> Siku za Mataifa zinakwisha, (tazama uchafu
> wake sasa) pamoja na kuhuzunishwa
> kwa mateso;
> Rudi kwenu, Ee, mliotawanyika.
> Siku ya ukombozi I karibu,
> Mioyo ya watu inazimia kutokana na hofu;
> Ujae Roho wa Mungu,
> Taa zenu ziwe zimetengenezwa na zinatoa
> mwanga dhaifu,
> Tazama juu, ukombozi wako umekaribia.
> (Hiyo ni sahihi.)
> Manabii wa uongo wanadanganya,
> wanakana Kweli ya Mungu,
> (je hilo ni sahihi!)
> Yesu aliye Kristo ni Mungu wetu.

Hawaamini Hilo. Wanazo namna zote za itikadi na vitu kama hivyo! …?… pia. Lakini nabii alisema … Au, mwandishi aliyevuviwa alisema:

> Tutatembea pale mitume walipokanyaga.

100 Mnakumbuka katika ono langu? Nilisema, "Kama watu wa Paulo wataingia, vivyo hivyo na wangu, kwa sababu nilifanya kama tu yeye alivyofanya." Ninakaa Nalo moja kwa moja.

Wale mamilioni walirusha mikono yao, wakisema, "Tumeweka matumaini yetu katika Hilo!" Nini? Tambua siku tunayoishi, wakati tunaoishi, ile ishara ya wakati tunaoishi. Inaweza ikawa wakati umepita kuliko tunavyofikiri. Mojawapo ya siku hizi, yule aliye nje aendelee kuwa nje. Yeye aliye ndani sharti aendelee daima kuwa ndani. Mlango utafunga.

Ikawa kuna baadhi hapa asubuhi hii ambao hawajawahi kuingia ndani bado, ee, katika Jina la Yesu, wapenzi wangu watu … Usimwangalie huyu mtumishi mjinga aliyesimama hapa, asiyejua kusoma, asiye na elimu,, asiyekuwa msomi; usiangalie hilo. Ila litazame Neno linalothibitishwa. Mtazame Roho Mtakatifu mkuu Ambaye analithibitisha Hilo kuwa ile Kweli. Tuko kwenye wakati wa jioni. Muda umesonga kuliko unavyofikiri. Usi- …

101 Wanawake acheni nywele zenu zikue. Dada, ondoa zile nguo chafu. Tupa mbali zile sigara. Kwani saa itakuja, ambayo, "Aliye mchafu, aendelee kuwa mchafu; na mwenye haki, aendelee kuwa mwenye haki. Yeye aliye ndani yuko ndani; yeye aliye nje yuko nje." Karibu kidogo na mstari, "Ikiwa mtu mwenye haki ataokolewa kwa shida, mwenye dhambi na mwovu atakuwa wapi, yule mkanaji wa ile Kweli, unajua, "wataonekana wapi?" Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

Sasa, katika Nuru ya saa hii tunayoishi sasa, ile Nuru ya siku tunayoishi sasa; ninyi mlio wa thamani na wapendwa, ninyi mnaotoka majimbo mbalimbali kote nchini, hebu sasa, na mimi pamoja nanyi, juu ya madhabahu haya, hebu tufanye mahesabu. Vipi kuhusu Roho wa Mungu mioyoni mwetu leo? Kumbukeni, ni Roho, asiye na hatia, msafi; fundisho lolote la kanisa, na kila kitu, kimeondolewa kabisa.

102 Usithubutu kujaribu kuongeza kwenye Hilo au uondoe kutoka Hilo. Kwani, kama ukijaribu kuweka mwenyewe, juu ya Hilo, sehemu yako inaondolewa kwenye kile Kitabu cha Uzima. Je, unajaribu kusema jambo fulani ambalo Roho hajasema? Unajaribu kulifanya Hilo lionekane kama limesema jambo fulani? Au, unalichukua tu hasa kile lilichosema, na kuliacha hivyo? Je, unaunga, unakata, unanasa, kufanya vitu ambavyo siyo sahihi? Umefanya hivyo?

Unasema, "Vema, sijisikii tu kama ningefanya hili. Au, labda, na-na-najua kanisa langu haliamini Hilo. 'Hilo ni neno la mtu mmoja tu kuhusu Hilo.'" Huyo Mtu mmoja ni Mungu. Biblia hapa inasema hupaswi kukata nywele zako. Hizi … Biblia ilisema hivyo. "Itakuwa kwamba wanawake watavaa mavazi kama mwanamume, na jinsi wangekuwa machukizo kwa Mungu." Jinsi Roho Mtakatifu alivyonena kupitia hilo, hiki chombo kinyenyekevu, kisichofaa kilichotokea tu kusimama katika kizazi kile ambacho yule Mfalme mkuu alisema, "Hili hapa kaburi Langu … Neno Langu. Namaanisha, Hii hapa Fimbo Yangu.. Chukua Fimbo Yangu, na uende, na ulete Ujumbe.

103 Najua madhehebu yalijaribu kulizuia Hilo, na kulizima Hilo, na kulifukuzilia mbali Hilo, na kulipiga mateke liende, na kila kitu. Lakini, kwa neema ya Mungu, niko barabarani mwangu, nikipiga kelele taifa hata taifa, mahali hadi mahali, kanisa hadi kanisa, "Tokeni kati yake!" Halipendwi na wengi, lakini ndilo lililo Kweli.

Je, utalipokea Hilo katika-katika-Roho ambayo liliandikwa ndani Yake? Utalipokea Hilo katika Roho ambayo limekuja ndani Yake? Ikiwa wewe bado … Hatuna nafasi kwa ajili ya madhabahu; moyo wako ndiyo madhabahu. Inua mkono wako, useme, "Mungu, nirehemu. Hebu Roho wa Mungu aje ndani yangu, akinihukumu sasa kwa dhambi zangu zote, na kukata tamaa kwangu, tabia zangu zote mbaya, na hasira zangu nyingi, na mizozo, na mapigano, na kuhamaki, na kila kitu ambacho nimekwishakuwa nacho. Na najua jambo fulani, kwamba roho yangu haijakomaa vizuri kwa ajili ya Mbinguni. Nikomaze, Bwana, katika hiki kitambo kifupi cha mwisho. Haya yanaweza kuwa mahubiri ya mwisho nitakayowahi kusikia. Huu inawza kuwa mara yangu ya mwisho kuusikia Ujumbe. Nainua mkono wangu. Mungu, nirehemu.

Mungu awabariki. Dazeni za mikono. Sasa, kwa kitambo kidogo tu cha maombi ya kimya kwa ajili yenu. Ninyi mlioinua mikono yenu, inaonyesha bado mna moyo. Inaonekana kwangu kama Roho bado anamwita mtu fulani.

104 Mungu mpenzi, Wewe Ambaye unajua mambo yote. Na Wewe uliumba vitu vyote kwa kusudi la vitu vyote, kwani baadhi vingehukumiwa, vingine vingepofushwa; vingine, "kama mfinyanzi alifinyanga kile chombo," kama Paulo alivyosema, "kimoja kwa heshima na kingine kwa aibu." Kimoja kilitengenezwa kiaibike, ilikuwa kuonyesha tu kile ambacho kingeheshimika. Lakini haiko mkononi mwa mfinyanzi kufanya kile Yeye atakacho? Je, haliko katika mpango wa kuchaguliwa tangu asili wa Mungu, kuita? "Yeye aliyemjua, alimwita, wale walioitwa, aliwahesabia haki. Na wale aliowahesabia haki, amewatukuza."

Labda baadhi yao hapa leo ni kama yule mwanamke pale kisimani, aliye mbali ndani ya uchafu, aliye mbali ndani ya kutokuamini, aliye mbali ndani ya desturi za mwanadamu, mafundisho ya kibinadamu. Labda ni kwa mara ya kwanza wamewahi kusikia haya mambo, lakini jambo fulani limeonya mioyo yao. Kuna wengi, mikono mingi iliyoinuliwa, Bwana. Hebu yule Mfinyanzi mkuu achukue kile kifaa sasa na kukifinyanga kuwa chombo cha heshima. Naamini kuna sababu fulani, Bwana, la sivyo wasingefanya hilo,

wasingesema hilo. Bado naamini, nashikilia kwa ajili yao.

105 Hebu mtumishi wako mnyenyekevu akusihi, Bwana. Hebu tusihi kwa ajili yao, kama ambaye amesimama kati ya walio hai na waliokufa; kama yule kule Sodoma alivyoomba kwa ajili ya Wasodoma, "Tokeni kwake! Tokeni kwake, upesi!"

106 Hebu waje, Bwana, kwa unyenyekevu na kwa upendo kwenye kiti cha enzi cha Mungu sasa, katika mioyo yao wakisema, "Yesu, kuanzia siku hii, na kuendelea Wewe utakuwa wangu. Naweka ahadi hili Kwako hapa sasa, nikiwa nimeketi hapa katika hiki kiti ambapo Roho Wako amenichoma. Ikiwa amenichoma nikiwa hapa, sina haja ya kwenda mbali zaidi ya hapa hapa. Hapa hapa ndipo Wewe ulinikuta; hapa hapa ndipo tunakwenda kufanya mapatano; hapa hapa kwenye hiki kiti cha pili, kiti cha tatu, kiti cha tano, chochotekile. Hapa hapa ndipo yatamalizika, kwa sababu hapa ndipo Wewe uliponihukumu,na hapa ndipo Wewe uliahidi kulirekebisha. Kwani ingawa ningekuwa najisi na mchafu, nitafanywa mweupe kama theluji. Naamini Neno Lako lote. Niko tayari kutembea ndani Yake, kuliamini Hilo, kulipokea. "Na sasa nafanya hili kwa ajili ya utukufu wa Mungu, nikijua kuwa maisha yangu hayanifai kitu, hayampendezi Mungu, hayawapendezi majirani zangu, hayafai kwa kitu kingine chochote; ni mazuri tu kwa Shetani, kunifanya kibaraka, kunitupa huko na huko, labda kuwa mwanasesere wa mtu fulani kumtunza, labda sanamu ya mwanamke fulani. Mungu, nifanye mtumishi Kwako." Unipe hilo,Bwana. Ninawakabidhi hawa Kwako sasa, katika Jina Lake Yesu Kristo, Mwana Wako.Tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, na mioyo yetu.

Namsikia Mwokozi wangu… (Kwa unyofu
wa moyo, rafiki.
Inaweza kuwa wakati wako wa mwisho.
Je, unaisikia ile Sauti ndogo?) ikiita,
Naweza (Nini Yeye anaita.... Nini kinakuita,
ikiwa Mwokozi wako ndiye lile Neno.)
Mwokozi anaita.
(Unapaswa ufanye nini? Uukane ulimwengu....)
"Niuchukue msalaba wangu na kumfuata,
kumfuata …
(Nimepuuza ubatizo katika Jina la Yesu,
Bwana.)...."
Nitakwenda Nayekupitia bustanini,
Nitakwenda (Pamoja Naye, wapi?
Kupitia majini, kupitia bustanini, kupita kokote,
nyumba ya maombi, katika kisima, popote.
Amua hilo.) ... kwenda Naye kupita bustanini,
Nitakwenda Naye,pamoja Naye njia yote.
Nitakwenda Naye kupita hukumuni, (iwe
Neno ni sahihi aukanisa ni sahihi.)
Nitakwenda................................

"Ama mimi niko sahihi,ama Yeye yuko sahihi. Dhambi yangu iko sahihi au Neno Lake ndilo lililo sahihi?" Uko mahali pa hukumu sasa. "Kile nilichoamini, je ni sahihi, au NenoLake, ndilo lililo sahihi? Je, ninadhani ni vema tu kuwa na nywele fupi, kuvaa kaptula? Je, nadhani ni vyema kuwa katika dhehebu?" Yeye alisema nini?

Nitakwenda Naye, pamoja Naye njia yote,
Sasa atakakoniongoza Yeye nitamfuata,

Mikono yangu iko juupia Bwana, Bwana popote ilipo, Ujumbe mwingine utahubiriwa wapi? Je, ni hapa,usiku huu, kule Afrika, Ujerumani, Switzerland? Ni mahali gani Bwana?

Popote Yeye … (popote Uniongozako, Bwana) …
mimi nitafuata.
Nitakwenda Naye, pamoja Naye njiani kote.

Sasa mkiwa mmeinamisha vichwa vyenu, je, utakwenda na Yeye kila mahali Yeye atakakokuongoza?

107 Je, utakwenda Naye wakati muda unavyozidi kuishia, watu wanakusumbua, wanakucheka, na kukufanyia mzaha? "Bado nitakuwa Naye, bado nitakwenda. Nitatembea moja kwa moja na Wewe, Bwana, popote Wewe ulipo. Bado nitasimama kuwa mwaminifu na mkweli. Nitasimama kuwa mwaminifu na mkweli, katika joto la mapambano. Kama nikianguka, utaniinua tena, Bwana. 'Yeye apotezaye uzima wake kwa ajili Yangu ataupata.'"

Kwa hiyo nitakwenda Naye, pamoja Naye.

Sasa wote wale wanaomaanisha hilo, kutoka mioyoni mwenu, hebu tuinue mikono yetu sasa, na mioyo yetu Kwake.

Aniongozako nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Aniongozako nitafuata,
Nitakwenda Naye, pamoja Naye njiani kote.
Atanipa neema na utukufu,
Atanipa …

Bwana Yesu, pulizia hizi leso sasa. Waponye hawa wagonjwa na wanaoteseka, Bwana. Tujalie Bwana. Wape uponyaji Bwana, katika Jina la Yesu.

Na kwenda nami, pamoja nami njiani mote.

108 Mnajisikia vyema sasa? Mnajisikia yote imekuwa tayari sasa? Ikiwa Yeye … Baragumu yake Bwana italia na wakati utakuwa umekwisha. Hiyo ni Baragumu ya mwisho sasa. Na wakati wa pambazuko la asubuhi njema, inayong'aa ya Milele. Hebu tuuimbe, sote sasa: Baragumu yake Bwana wakati ikilia. (Tupe sauti.)

Baragumu yake Bwana wakati ikilia,
Na wakati utakuwa umekwisha;
Wakati wa pambazuko la asubuhi njema,
inayong'aa ya Milele;
Hapo waliokombolewa kutoka duniani
watakusanyika, kule ng'ambo ya pili
Majina yatakapoitwa kule nitakuwako.

Wakati majina yaitwa pokule,
Wakati majina yaitwa pokule,
Wakati majina yaitwa pokule,
Wakati majina yaitwapo kule, nitakuwapo

Katika asubuhi ileinayong'aa isiyo na mawingu
waliokufa katika Kristo wafufukapo
Tutashiriki na fahariyake ya ufufuo;
Na kushiriki utukufu wa kufufuka Kwake;
Wakati maisha yote yatakuwa yamekoma
na kazi yetu hapa duniani itakuwa imekwisha,
Majina yaitwapo kulenitakuwapo.

Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule, nitakuwapo.

109 Hebu tuinue mikono yetu, tuseme, "Kwa neemaYako, Bwana." Kwa neema Yako Bwana! [Kusanyiko, "Kwa neema Yako Bwana."-Mh.] Sasa,sisi ni ndugu na dada katika Kristo. Hebu tugeuke tu na kupeana mkono na mtu fulani pembeni mwako, na useme, "Kwa msaada wa Mungu, majina yaitwapo kule...."

Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule, nitakuwepo.

Tunasubiri nini?

Wakati ile Baragumu (ile ya mwisho!)
Bwana, italia, na wakati hautakuweko tena,
(tumeingia Umilele,"Kwa kitambo kidogo,
kufumba na kufumbua jicho.") na njema;
Hapo waliokombolewa kutoka
duniani watakusanyika
kule ng'ambo ya pili,
Wakati majina yaitwapo kule, nitakuwepo.

Hebu tuimbe tu!

Wakati majina yaitwapo kule,

Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule,
Wakati majina yaitwapo kule, nitakuwepo.

110 Loo, je, huo ni wakati ulioje! Ukitemebea tu mwenyewe siku moja, na hapa anatokea mtu fulani. "Nani? Mama!" Amina! "Haitakuwa muda mrefu sasa." Dakika chache tu, umebadilishwa. Na tutakuwa … tutakutana nao, ndipo tutanyakuliwa nao pamoja, kumlaki Bwana hewani. Loo, katika kitambo kidogo, katika kufumba na kufumbua jicho. Unasema, "Huyu hapa Ndugu Seward, ndugu wa zamani aliyewahi kuwa hapa kanisani! Mbona huyu hapa Ndugu DeArk. Huyu hapa Ndugu Fu-… Mbona, tazama hapa, wamenizunguka kote! Kuna jambo gani? Kwa dakika chache tu hapa … Najua wamekwishakunitokea. Haitachukua muda mrefu sasa. Nitabadilishwa sasa, kwa kitambo kidogo tu, kwa kitambo kidogo tu." Loo, ndiyo! Na asubuhi ya Milele ikifika, inang'aa na nzuri. Mawingu yote yasiyoweza kuelezeka …

111 Kama Yeye alivyosema, "Israeli, ingawa amekuwa kama mawingu ya asubuhi, umande , na haki yako inaondoka." Na inapokuwa imeondoka yote kuingia kwenye Nuru ya Mwana Ambaye hushikilia yote, amina,ndipo, "Majina yaitwapo kule, nitakuwapo." Vema, hadi usiku huu:

Hata tuonane! Hata tuonane!,

Hatujui ni wakati gani hili litatokea marafiki. Imekuwa hadithi, muda mrefu, lakini ni Kweli, naitatukia. Tuko kwenye wakati hasa sasa.

Hata tuonane, hata tuonane, hata …
(Kwa neema ya Mungu
tunatumaini, saa moja na nusu usiku huu.),
Mungu awe nanyi hatatuonane tena.

Hebu tusimame sasa kwa miguu yetu.

112 Ee, si jambo zuri sana? "Haya ni makao ya Kimbinguni katika Kristo Yesu." Siwezi kubadilishana hili na chochote kile. Mnajua jinsi ninavyopenda kuvua samaki na jinsi ninavyopenda kuwinda, kwa sababu namwona Mungu kule nyikani. Napenda hilo. Lakini, ee, siwezi kubabadilishana dakika moja ya hili kwa ajili ya furaha ya ushiriki wangu nyikani wa miaka mamia. Dakika moja kwa ajili ya hili, huo ni utoshelevu.

Mungu, umba uamsho ndani mwangu. Nifanye mimi niwe uamsho. Hebu kila mmoja wetu awe uamsho, uamsho ndani yangu. Nifanye Bwana, niwe na njaa, nifanye niwe na kiu. Umba ndani yangu Bwana, kile kinachohitajika ndani yangu. Nifanye, kuanzia saa hii na kuendelea, niwe Wako; mtumishi aliyewekwa wakfu zaidi, mtumishi mzuri zaidi, aliyebarikiwa na Wewe zaidi; mwenye uwezo zaidi, mnyenyekevu zaidi, mwema zaidi, anayetaka kutenda kazi zaidi; mwenye kutazama zaidi yale mambo yakini, na kusahau yale mambo yaliyopita, na yasiyofaa. Hebu nisonge kuelekea kwenye alama ya mwito mkuu wa Kristo. Amina! Hiyo ndiyo shauku yetu, sivyo?

Vema, hebu, hadi tuonane usiku huu. Hebu tulichukue Jina la Yesu pamoja nasi, kila mmoja wenusasa.

Peleka-peleka Jina laYesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Itakufurahisha na kukufariji,
Peleka uendako.

Jina la Thamani, Ee lililo tamu!
Tumaini la dunia naraha ya Mbinguni;
Jina la Thamani, Ee lililo tamu!
Tumaini la dunia naraha ya Mbinguni.

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu.

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao kutoka kila mtego
Wakati majaribu yanapokukusanyikia …
Pumua hilo Jina takatifu katika maombi....

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7